**Mtoto** wa miaka sita alivyouawa kikatili, mwili watolewa viungo

UKURASA 3



**RIPOTI:** Mauaji ya wivu mapenzi yanavyoacha simanzi kubwa kwa jamii

UKURASA 4


Nipashe Spotika

USAJILI 10 GHALI ZAIDI MAN UNITED UK. 12-13

NYOTA WANAOLIPWA MISHAHARA MIKUBWA EPL

ISIKUPITE

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Julai 26, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580653

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Hatima ya Mbowe bado kitendawili

UKURASA 2



Freeman Mbowe

## 'Level seat' na barakoa lazima, harusi sasa masharti magumu

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### WAUGUZI, WAKUNGA 50 WAFUTIWA LESENI

SERIKALI imewafutia leseni na vibali vya usajili wauguzi na wakunga 50, waliokuwa wakifanyakazi katika vituo mbalimbali vya afya, baada ya kubainika wameghushi nyaraka hizo. Akizungumza katika mahafali ya pili ya kuwaapisha...

UKURASA WA 5

### TAASISI YA MKAPA YASAIDIA BARAKOA ZA MIL. 50/-

TAASISI ya Benjamin Mkapa imetoa msaada wa barakoa zenye thamani ya Sh. milioni 50 kwa ajili ya kusaidia mapambano ya ugonjwa wa corona jijini Mwanza. Barakoa hizo ambazo zimetolewa kwa...

## Mapigano ya wafugaji, wakulima yaua watatu

UKURASA 3

MICHEZO AZAM YATAJA SABABU YA KUWAACHA WA KIMATAIFA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Baadhi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Seka iliyoko Kata ya Nyamrandirira, Wilaya ya Musoma mkoani Mara, wakiendelea na masomo. Shule hiyo mpya ilijengwa kwa nguvu za wananchi na kufunguliwa rasmi Julai 5, mwaka huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yakaza masharti kuikabili corona

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imetoa mwongozo mpya wa kupambana na corona, huku ikipiga marufuku mikusanyiko mikubwa ya kijamii, kama sherehe, kisiasa na kidini isiyo ya lazima hadi ugonjwa huo utakapodhibitiwa na taarifa kutolewa rasmi.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Abel Makubi, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Kutokana na mwenendo wa ugonjwa wa corona nchini, kamati ya wataalamu imeainisha maeneo mahususi yanayohitajika kutiliwa mkazo kupitia afua za kupunguza msongamano katika jamii, lengo ni kukata mnyororo wa maambukizi katika ngazi ya kaya na jamii," alisema.

"Mwongozo huu utawawezesha wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi na kijamii sambamba na kubadili tabia zao huku wakizingatia mbinu za kujikinga na ugonjwa, kwa kupata elimu ya kutosha na kujiwekea utaratibu wa kudhibiti ugonjwa kutokusambaa kwenye jamii."

Alisema pale ambapo patahitajika kufanyika shughuli za mikusanyiko, kutatakiwa kuombwa kibali maalum.

"Maeneo yanayoleta mikusanyiko ni yale ya huduma za kijamii, kibiashara, kiuchumi, kiofisi, ambayo ni mojawapo ya vyanzo vya kusambaa kwa maambukizi katika jamii. Mwongozo huu unalenga kudhibiti ugonjwa huu bila kuathiri shughuli za kiuchumi na maisha ya kawaida ya kijamii ya wananchi."

Pia, alitaka wasafiri wawezeshwe kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka kabla ya kuingia kwenye vyombo hivyo vya usafiri.

Mwongozo huo unawataka viongozi wa mtaa husika kuhakikisha kila kituo kunawekwa vyombo vya kuhifadhia maji na sabuni vya kutosha.

Kwenye vituo vya mabasi, unaelekeza uongozi wa vituo hivyo, kusimamia uwapo wa vifaa vya kunawia kwa maji tiririka na kuhakikisha abiria wote wananawa mikono.

Unawaelekeza pia wamiliki wa vyombo vya usafiri kuhakikisha wanaweka vipukusi vya kutakasa mikono katika vyombo vya usafiri na kusimamia uvaaji barakoa.

**BARAKOA LAZIMA**

"Abiria wote waendelee kuelimishwa kuhusu umuhimu wa kutosongamana ndani ya vituo vya mabasi kupitia walinzi getini, wahudumu wa mabasi na askari wa usalama wa barabarani.

"Stendi zihakikishe zinatoa ujumbe wa kuelimisha jamii ya wasafiri mara kwa mara kupitia vipaza sauti, na wanapokuwa safarini, madereva na wahudumu wa vyombo vya usafiri wahakikishe ujumbe wa kuelimisha unatolewa kwenye chombo mara kwa mara."

**MARUFUKU ABIRIA KUSIMAMA**

"Vyombo vya ulinzi na usalama vihakikishe magari ya usafiri wa umma wanapakia abiria kulingana na idadi ya viti pasipo kusimama, kwa magari maalumu yenye nafasi kubwa kama mwendokasi, inapolazimika kusimama basi kila abiria avae barakoa na kuachiana angalau umbali wa nusu mita," alisema Profesa Makubi.

**UPIMAJI**

"Upimaji wa dalili za ugonjwa wa corona na taratibu getini wakati wa kuingia/kutoka ndani ya mabasi. Kupima joto mwili kwa kutumia 'thermoscanners' ufanyike getini na kwenye mabasi."

**NYUMBA ZA IBADA**

Mwongozo huo mpya unaelekeza nyumba za ibada kukaguliwa mara kwa mara, kuweka vifaa vya kunawia na maji tiririka, waumini kuvaa barakoa, na kukaa umbali wa mita moja kutoka mtu mmoja na mwingine na kuwapo na utaratibu wa utakasaji wa viti, meza na maeneo wanayokaa kabla na baada ya ibada.

"Wazee, watoto na wale wote wenye matatizo ya kiafya yanayotambulika ikiwamo kisukari, shinikizo la damu, saratani, wanashauriwa kujiepusha na ibada zenye mikusanyiko ya watu wengi na wachukue tahadhari zote muda wote," alisisitiza.

"Ibada ziwe za muda mfupi usiozidi saa mbili. Huduma zinazohusisha kugusana ziepukwe. Kuwapo na ujumbe wa mara kwa mara kwa ajili ya kuwakumbusha waumini kuhusu namna ya kujikinga."

**KUMBI ZA STAREHE**

"Maeneo ya baa, migahawa, hoteli, kumbi za starehe, mikutano, harusi na sherehe mbalimbali kimsingi baadhi ya shughuli za kundi hili zinafaa kuangaliwa iwapo ni muhimu, za lazima au zisubiri hali itengemae. Iwapo ni muhimu na lazima kuwe na kipima joto kwa wote wanaoingia kupata huduma kwenye eneo husika."

"Sherehe zote za harusi kufanyika nje ya kumbi au kama zinafanyika ukumbini, ziwe za muda fupi, wageni waalikwa wawe wachache kuruhusu ukaaji wa mita moja au zaidi."

**VITUO VYA AFYA**

Mwongozo huo unaelekeza kwamba wagonjwa wa nje wasio na dharura waonwe kwa kupangiwa tarehe maalumu ili kuzuia mrundikano kwa wagonjwa kwa wakati mmoja na kwamba wagonjwa wenye magonjwa sugu wapewe dawa za angalau miezi miwili.

**VITUO VYA POLISI NA MAGEREZA**

Mwongozo huo unaelekeza vituo hivyo kutoa kipaumbele cha dhamana kwa mahabusu wenye makosa yanayodhaminika kisheria ili kupunguza msongamano na kuruhusu ndugu mmoja tu kumtembelea mfungwa katika siku iliyotengwa na kuwataka wasikilizaji wa kesi kuvaa barakoa na kukaa kwa umbali.

**MASOKONI**

Mwongozo kwenye masoko unatelekeza halmashauri ziandae timu za kukagua maeneo hayo, ikiwa ni pamoja na kutumia viwanja vya mipira wa miguu au maeneo yoyote yaliyo wazi kwa ajili ya huduma za masoko au kushushia bidhaa.

# Hatima ya Mbowe bado kitendawili

**Na Richard Makore,** MWANZA

HATIMA ya Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, haitajulikana kutokana na Jeshi la Polisi mkoani Mwanza kutoweka wazi lini atarejeshwa kwa ajili ya kuhojiwa kama lilivyoahidi awali.

Wiki iliyopita Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Ramadhani Ng'anzi, alithibitisha kwamba walimkamata Mbowe alfajiri ya Jumatano na kumsafirisha kwenda Dar es Salaam kwa mahojiano kwa makosa mengine aliyokuwa akituhumiwa nayo.

Akizungumza na waandishi wa habari siku hiyo, alisema Mbowe baada ya kumaliza kuhojiwa Dar es Salaam angerudishwa jijini Mwanza kwa ajili ya kuhojiwa na jeshi hilo.

"Suala la Mbowe bado linashughulikiwa Dar es Salaam, lakini sijajua ni lini atarudishwa, wao (Dar) ndiyo watasema," alisema.

Aidha, taarifa ya maandishi iliyotolewa siku hiyo haikuwa na jina la Mbowe halikuwamo kama mtuhumiwa aliyekamatwa jijini Mwanza pamoja na viongozi wenzake na wanachama.

Jeshi hilo lilisema siku ya Jumatano lilikamata watu 15 ambao ni viongozi na wafuasi wa CHADEMA jijini Mwanza kwa madai ya kutaka kufanya mikusanyiko ya kudai ya katiba mpya iliyopigwa marufuku na serikali.

Wafuasi na viongozi hao 15 wa CHADEMA baada ya kukaa mahabusu kwa siku tatu, Jumamosi waliachiwa bila kuambiwa ni lini watatakiwa kuripoti tena Polisi.

Alisema waliachiwa hadi upelelezi utakapokamilika watawaita tena ili kuwafikisha mahakamani, ingawa hakusema ni lini.

Wiki iliyopita msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, alisema Mbowe anakabiliwa na makosa ya ugaidi ya kupanga njama za kuua viongozi wa serikali.

Alipotafutwa jana kwa njia ya simu kuzungumzia kinachoendelea kuhusu Mbowe, pamoja na Kamanda wa Kanda Maalum, Jumanne Muliro, simu zao ziliita bila kupokelewa.

HABARI KITAIFA

# Mapigano wakulima, wafugaji yaua watatu

**Na Said Hamdani,** LINDI

WATU watatu, wawili wafugaji na mmoja mkulima wakazi wa Kijiji cha Nanjirinji 'B' Wilaya ya Kilwa katika Mkoa wa Lindi, wamekufa katika mapigano yaliyosababishwa na mifugo kuingia shambani na kula mazao.

Mkulima aliyeuawa ametajwa jina wakati wafugaji majina yao hayajafahamika, huku Jeshi la Polisi likiwashikilia watu 55.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho, Kassimu Maimula na mjumbe wake, Abdallah Chande, walisema mapigano hayo yalitokea Julai 20, mwaka huu majira ya mchana.

Mmoja wa mashuhuda, Fatuma Limbapa, alimtaja mkulima aliyeuawa ni Chande Magoma.

Mashuhuda ambao hawakutaka majina yao kutwajwa, walisema siku hiyo, wafugaji walipeleka shambani kwa Magoma mifugo yao na kula mahindi.

Walisimulia kuwa alipowauliza kisa cha kugeuza mazao yake kuwa chakula cha ng'ombe walimwangalia bila kusema chochote wala kuondoa mifugo.

Walisema kitendo cha wafugaji kutowaondoa mifugo yao, Magoma aliamua kuwafukuza ng'ombe kutoka ndani ya shamba ndipo ugomvi ulipoanza na wakaanza kushambuliana maeneo mbalimbali ya mwili kwa kutumia fimbo walizokuwanazo, hali iliyomfanya mkulima aishiwe nguvu na kuanguka chini na kupoteza fahamu.

Walisema kitendo kile kiliwasukuma watu waliokuwapo kutoa msaada wa kumwokoa na kumkimbiza Kituo cha Afya Nanjirinji kupata matibabu, lakini kutokana na kupata majeraha makubwa, alihamishiwa Hospitali ya Ruangwa.

Walisema walipofika eneo la Kijiji cha Mbekenyera, Wilaya ya Ruangwa, Magoma alifariki dunia.

Walisema Fatuma Limbapa, mke Magoma, alipohoji kutaka kufahamu sababu za kumpiga mumewe, wafugaji hao, walimchomolea kisu, huku wakimtaka akae kimya vinginevyo na yeye watamteketeza na kuwajibu yupo tayari kwani haogopi kifo.

Aidha, ilidaiwa wafugaji hao baada ya kuona kundi la watu wakifika eneo hilo, waliingia ndani ya nyumba ya Magoma na kupora bunduki aliyokuwa anaimiliki na kuondokana yao kuelekea kusikojulikana.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, ACP Mtatiro Kitinkwi, amethibitisha kutokea vurugu hizo zilizoambatana na mauaji ya watu watatu na kutaja jina la Magoma, huku akisema wafugaji wawili waliopoteza maisha majina hayajafahamika.

Alisema watu 55 wanashikiliwa na Polisi kwa mahojiano zaidi ili kufahamu kiini cha mapigano hayo, na kwamba watakaobainika kuwa chanzo watafikishwa mahakamani.



Rais wa Chama cha Wahasibu Tanzania (TAA), Godvictor Lyimo (kushoto), akiwashukuru wanachama wa chama hicho kwa kumchagua kukiongoza, (kulia) ni Makamu wa Rais, Victorius Kamuntu, (katikati) Ofisa Mtendaji Mkuu, Baraka Ambangile. Uchaguzi huo ulifanyika mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wauguzi, wakunga 50 wafutiwa leseni

**Na Moshi Lusonzo,** KIBAHA

SERIKALI imewafutia leseni na vibali vya usajili wauguzi na wakunga 50, waliokuwa wakifanyakazi katika vituo mbalimbali vya afya, baada ya kubainika wameghushi nyaraka hizo.

Akizungumza katika mahafali ya pili ya kuwaapisha wauguzi na wakunga wapya mjini Kibaha, mkoani Pwani jana, Msajili wa Baraza la Wauguzi na Wakunga nchini (TNMC), Agnes Mtawa, alisema wamegunduliwa baada ya kuanza kutumia mfumo wa teknolojia ya kanzidata.

Aidha kwa mwaka huu pekee, jumla ya malalamiko 30 dhidi ya watumishi waliokiuka maadili na miongozo ya kitaaluma yamepokelewa.

Mtawa alisema baada ya kufanya uchunguzi baraza hilo lilitoa onyo kwa watumishi wa afya 17, watano walisimamishwa kazi na mmoja alifutwa katika daftari la usajili.

Alisema katika kukabiliana na hali hiyo, Baraza linatengeneza mwongozo wa kushughulika na malalamiko utakaosaidia kujenga uwezo wa wadau wa uchukuaji hatua wanapoona kuna uvunjaji wa maadili ya kitaaluma.

"Baraza linahusika kwa karibu katika kusimamia mafunzo ya wauguzi na wakunga kwa sababu taaluma hii si elimu pekee, bali ni tabia na matendo yanayofuata maadili," alisema Mtawa.

Msajili huyo alisema jumla ya wauguzi na wakunga wapya 2,173 wamepewa leseni na vibali vya usajili baaada ya kufanya mtihani wa mchujo unaosimamiwa na baraza hilo. Tangu kuanza kwa sheria ya usajili kwa wauguzi na wakunga wenye uwezo, jumla ya watu 38,303 wamefanya mitihani na kati ya hao 27,095 walifaulu.

Hata hivyo, kumekuwapo na ufaulu hafifu kwa wahitimu wanaomaliza mafunzo ya uuguzi na ukunga, kutokana na kuwapo kwa miongozo, usimamizi na uendeshaji hafifu wa mitaala.

Katika hotuba ya Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Alfello Sichwalwe, ambayo ilisomwa na mganga mkuu wa Pwani, Dk. Gunini Kamba, aliwataka wahitimu hao kwenda kufanya kazi kulingana na mafunzo yao ili kuepukana na malalamiko.

## Mtoto alivyouawa kikatili, mtuhumiwa mmoja ashikiliwa

**Na Said Hamdani,** LINDI

MTOTO Mwilu Ahamadi (6) mkazi wa Kijiji cha Nampungu, Kata ya Mingumbi, Wilaya ya Kilwa mkoani Lindi, amekutwa amekufa baada ya kutoweka nyumbani kwao wiki moja iliyopita, huku baadhi ya viungo vya mwili wake vikiwa vimeondolewa. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, ACP Mtatiro Kitinkwi, amethibitisha kutoa kwa tukio hilo na kueleza kuwa wanamshikilia mtu mmoja kutokana na kifo cha mtoto huyo.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wakazi wa kijiji hicho, waliojitambulisha kwa majina ya Hemedi Ismail, Mohamed Juma na Elena Emmanuel, wameeleza kwamba mtoto huyo alitoweka nyumbani tangu Julai 15, mwaka huu.

Walisema siku hiyo mtoto huyo akiwa anacheza na wenzake, aliondoka nyumbani kwao na hakuweza kurejea tena.

Walisema kwamba kitendo cha kutorejea nyumbani kwa mtoto huyo, wananchi walianza kumtafuta maeneo mbalimbali bila mafanikio.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Nampungu, Kassimu Macho, alithibitisha kupotea kwa mtoto huyo na kueleza kuwa alipatikana Julai 21, mwaka huu, akiwa amefariki huku baadhi ya viungo vyake vikiwa vimeondolewa.

Alitaja viungo vilivyoondolewa ni pamoja na sikio la kulia na mguu wa kulia ambavyo vimekatwa.

Macho alisema mwili wa mtoto huyo ulionekana baada ya baba mdogo wa mtoto huyo, Hemedi Chauleni, kupandisha mashetani na kumtaka mdogo wake aliyetajwa kwa jina la Seifu waende moja ya njia zilizopo katika kijiji hicho na kufanikiwa kuukuta mwili wake ukionekana umenyongwa shingo.

"Baada ya kumtafuta kwa siku zote tano bila mafanikio, baba mdogo wa yule kijana, ghafla akapandisha mashetani na kumtaka Issa ampeleke upande huu," alisema Macho.

Alisema Hemedi Chauleni, ndiye aliyesaidia upatikanaji wa mwili wa mtoto huyo baada ya kupandisha mashetani, hata hivyo Jeshi la Polisi linamshikilia kwa mahojiano zaidi.

KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**ATHUMANI RAMADHANI GENDAEKA** Anatangaza kupotelewa kwa ofa yake ya kiwanja chenye PLOT namba **132 BLOCK T KARUME** Kwa yeyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Rb Namba: **MOR/MOR/RB/366042/2021**

116372302

IMARA BRAKE LININGS TABATA DAMPO

MALI MPYA IMEWASILI.

Gundi (Bostik) kwa Sh. 130,000/- Kwa ujazo wa lita 5.

Wasiliana nasi kwa simu namba 0783 277 909; 0714 475 898.

116367002

MAKALA MAALUM

# Mauaji wivu wa mapenzi yanavyoacha simanzi -1

## •Polisi, LHRC na wanasaikolojia wanena

Na Maulid Mmbaga

MATUKIO ya ukatili wa mauaji, unajisi na ubakaji dhidi ya binadamu wengine yanaongezeka sababu kubwa ikitajwa ni wivu wa kimapenzi kiasi cha kugharimu maisha ya wengine na kuacha watoto yatima, ulemavu na uadui kati ya ndugu na ndugu au wanajamii.

Kutokana na kuongezeka kwa matukio hayo, Nipashe imefanya utafiti kwa kuangazia matukio yaliyotokea kuanzia Juni mwaka 2020 hadi Julai mwaka huu, na kubaini kuwa matukio yaliongoza ni ukatili kati ya wapenzi na kwa mwaka jana, kulikuwa na matukio 75 huku mwaka huu yakiwa 56.

Aidha, matukio ya wivu wa kimapenzi yalikuwa 38 na kati yake mwaka 2020 yaliongoza yalikuwa 23 na mwaka huu 15, huku matukio ya ubakaji ( 27) ambayo ni 20 mwaka jana na saba mwaka huu.

Kwa mwaka jana idadi ya matukio kila mwezi kwenye mabano ni Juni (12), Julai (6), Agosti (13), Septemba (12), Oktoba (13) Novemba (11) na Desemba (8).

Kwa mwaka huu, Januari uliongoza kwa kuwa na matukio 14, ukifuatiwa na Aprili matukio tisa, Machi na Juni ulikuwa na matukio nane huku mwezi huu ambao umebakisha siku tano ukiwa na matukio 10 na Februari ukirekodi machache yaani manne.




**TAKWIMU ZA POLISI**

Julai 20, mwaka huu, Jeshi la Polisi nchini lilitoa takwimu za nchi nzima kuanzia Mei hadi Juni mwaka huu, zikionyesha watu 5,429 walikamatwa kwa kujihusisha na uhalifu.

Matukio ya mauaji yalikuwa 275 na kati yake wivu wa mapenzi ni 21 imani za ushirikina ni 23 na 231 sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujitafutia kipato kwa njia za kiuhalifu.

**MWANASAIKOLOJIA**

Mwanasaikolojia na Mhadhiri Msaidizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Magolanga Shagembe, akifafanua kwamba kiini cha matukio ya kuuana miongoni mwa wachumba na wanandoa yanayoripotiwa kwa wingi nchini inachangiwa na uchumba na ndoa nyingi kujengwa kwa msingi aliouita mbovu wa kukidhi haja ya kimwili.

“Uhusiano unavunjika kwa sababu yanajengwa katika msingi mbovu. Vijana wengi wanaingia katika mahusiano kwa lengo la kikidhi haja zao za kingono tu na siyo mapenzi ya dhati,” alibainisha.

“Ili uhusiano uwe na tija, ni lazima kuwe na vitu vya ziada vya kuwaunganisha wahusika, tofauti kabisa na kuishia kufanya mapenzi tu, mfano kushauriana mambo ya shule, kazi na maisha kwa ujumla,” alisema.

LHRC

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema kumekuwa na mwendelezo wa matukio ya ukatili na mauaji yanayotokana na wivu wa mapenzi, watu kujichukulia sheria mkononi na mengine yanayohusishwa na imani za kishirikina.

Alisema utafiti uliofanywa na LHRC mwaka 2019 ulibaini matukio takribani 12 ya mauaji ya wanawake, yaliyofanywa na wenza wao, huku matukio nane yakihusishwa na wivu wa kimapenzi.

Pia kwa mwaka 2020, idadi ya matukio ya mauaji ya wanawake yaliyofanywa na wenza wao, yaliongezeka hadi kufikia 32 huku 23 yakisababishwa na wivu wa mapenzi, na kutoa wito kwa wananchi kulinda haki wengine.

**MWAKA JANA**

Kwa mwaka jana, matukio yaliyoripotiwa ni Juni 2, mchungaji wa Kanisa la Mlango wa Ukombozi, Gairo mkoani Morogoro, Joseph Gervas (28), alifikishwa mahakamani kwa tuhuma za kumbaka na kumpa mimba mwanafunzi.

Siku hiyo hiyo, watoto wawili wa miaka minne waliuawa mkoani Pwani na Shinyanga kwa kukatwa mapanga, wa kwanza chanzo ni wivu wa mapenzi kwa mke mkubwa Sofia Mariam (28) kukosa mtoto wakati mke mdogo ana mtoto, na wa Shinyanga chanzo hakikubainishwa.

Juni 3, watu watatu walishikiliwa Kinondoni kwa tuhuma za kumuua dereva teksi, Joseph Mwenda na kumzika maeneo ya karibu na Shule ya St. Mary’s Mbezi Makonde kisha kumwibia.

Siku hiyo hiyo, Justine Joseph mkazi wa Wilaya ya Kyerwa, alishikiliwa kwa tuhuma za kumuua mama yake kwa kumshambulia kwa kipigo, kumbana shingo hadi kufa, kwa madai ya kuto mhudumia mgonjwa ambaye ni baba yake.

Juni 14, Mahakama ya Mkoa wa Lindi ilimhukumu Kasimu Chilimba (18), mkazi wa Kata ya Nyengedi kuchapwa viboko 12 baada ya kukutwa na kosa la kumbaka mwanafunzi.

Juni 16, mkazi wa Kimara mkoani Dar es Salaam, Erick Bubelwa, alishikiliwa na Polisi kwa tuhuma za kumuua mke wake, Mercy Mkambala (30) chanzo wivu wa kimapenzi.

Juni 18, 2020, mkazi wa Bunda jina lake halikubainishwa, alishikiliwa kwa tuhuma za kuwazalilisha kijinsia na kuwabaka mfululizo watoto wake watatu na kumpa mimba wa miaka 13.

Juni 19, aliyekuwa mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Chisegu, Masasi mkoani Mtwara Mohamedi Mboloma alikutwa amejinyonga msituni, baada ya kutoweka nyumbani kwake siku tatu.

Juni 20, walimu katika kijiji cha Chihwanga, Kata ya Itaragwe wilayani Gairo, mkoani Morogoro, mwalimu mmoja aliuawa na mwingine kujeruhiwa kwa madai ya wivu wa mapenzi.

Juni 23, baba mmoja mkazi wa Bunda, alidaiwa kumbaka mtoto wake wa kumzaa kwa ahadi ya kumpa Sh. 5,000.

Juni 25, mwanafunzi wa Chuo cha Utumishi Kange, kilichopo mkoani Tanga Waziri Ramadhan, alituhumiwa kwa kumuua mwanafunzi mwenzake Hussein Daudi, baada ya kumkuta kwenye chumba cha rafiki yake wa kike.

Juni 30, wafanyakazi wanne wa kiwanda cha uchenjuaji Madini ya Dhahabu (Plant) katika mgodi mdogo wa Mtambalale, kijiji cha Wisolele, wilayani Kahama waliuawa kwa kucharanga na mapanga na watu wasiojulikana, na sababu ya tukio hilo ni kutaka kupora mali.

Julai Mosi, Sinoni mkoani Arusha, ndugu wawili wa familia moja walituhumiwa kumuua mdogo wao, Mandela Malisa kwa madai ya kumkuta amelala kwenye chumba cha baba yao mzazi ambaye ni marehemu, chanzo kikidaiwa kugombania nyumba ya urithi.

Julai 9, Juma Kisinza (50) alihukumiwa kifungo cha miaka 30 jela kwa kosa la kumbaka mwanafunzi mwenye umri wa miaka 13.

Julai 8, Chalinze mkoani Pwani, mfanyakazi za ndani Yasini Abdalla (35) aliuawa na wananchi wenye hasira kali baada ya kudaiwa kuwaua watoto wawili wa familia moja na kumjeruhi mama yao chanzo kutoelewana.

Julai 10, Daria Frank (55) mkazi wa Mamba wilayani Moshi alishikiliwa na polisi mkoani Kilimanjaro kwa tuhuma za kumuunguza na moto mtoto wa miaka sita.

Julai 21, Alistides Crizostom (40) mkazi wa Karagwe mkoani Kagera alishikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani humo kwa tuhuma za kumuua mke wake Donina Alistides (53), baada ya kufumania na mwanaume mwingine.

Julai 31, mwanafunzi wa darasa la tano katika Shule ya Msingi Kilango, Kahama mkoani Shinyanga alidaiwa kubakwa siku ya mkesha wa harusi. Agosti 4, kijana Ulandi Dotto (28) mfugaji mkazi wa Mbarali mkoani Mbeya alifariki dunia baada ya kupigwa risasi na askari wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) baada ya kupitisha mifugo yake ndani ya eneo la hifadhi.

Agosti 6, mfanyakazi za ndani Magige Thomas (21) mkazi wa Tarime mkoani Mara, alihukumiwa kutumikia kifungo cha maisha jela kwa kosa la ulawiti.

**ITAENDELEA KESHO**

## HABARI KITAIFA

# Korti yatupa rufani hukumu ya kunyongwa hadi kufa

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Rufani imetupilia mbali maombi ya mapitio yaliyowasilishwa na Said Mapeyo, aliyehukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kosa la mauaji ya kukusudia.

Uamuzi wa mahakama hiyo ulitolewa na jopo la majaji watatu, Jaji Austine Mwarija, Jaji Mary Levira na Jaji Dk. Paul Kihwelo, baada ya kupitia sababu za mapitio na hoja zilizowasilishwa na pande zote mbili.

Mapeyo anayetakiwa kuendelea na adhabu aliyopewa, aliomba mahakama hiyo ifanye mapitio ya hukumu iliyotolewa na jopo la majaji watatu wa Mahakama ya Rufani waliobariki adhabu iliyotolewa na Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam Februari mwaka 2020.

Katika maombi ya mapitio Mapeyo aliwasilisha sababu tatu za kufanya hivyo, ikiwamo kwamba hakupewa nafasi ya kusikilizwa na Mahakama ilikosea kwa kushindwa kumuita daktari aliyefanyia uchunguzi mwili wa marehemu kufika kutoa ushahidi.

Mapeyo anadaiwa kumuua Mussa Marco maarufu Mhagama, mwili wa marehemu huyo ulikutwa bila kuwa na kichwa, alishtakiwa mwaka 2017 na kuhukumiwa adhabu ya kunyongwa hadi kufa mwaka 2020.

Jopo baada ya kupitia hukumu hiyo, kupitia hoja za mrufani aliyejiwakilisha mwenyewe na hoja ya Wakili wa Serikali, Deborah Mushi, ilifikia uamuzi kwamba hoja zote za mapitio hazina msingi.

Mahakama ilisema kwamba sababu zilizotolewa hazina sifa ya kutolewa katika maombi ya mapitio, na kwamba Mapeyo alitaka kupitishia sababu za rufani kwa mlango wa nyuma.

"Hoja kuhusu uchunguzi wa mwili wa marehemu ni kwamba uchunguzi wa mwili ulifanyika bila kichwa, adhabu iliyotolewa ilikuwa sahihi kulingana na ushahidi uliotolewa katika mahakama hiyo ya chini.

"Katika hoja zilizowasilishwa hakuna hoja ya kuathiri hukumu ya Mahakama Kuu, maombi ya mapitio hayana msingi, Mahakama inayatupilia mbali," lilisema jopo hilo katika uamuzi wake.

# Taasisi ya Mkapa yasaidia barakoa za mil. 50/-

**Na Richard Makore,** MWANZA

TAASISI ya Benjamin Mkapa imetoa msaada wa barakoa zenye thamani ya Sh. milioni 50 kwa ajili ya kusaidia mapambano ya ugonjwa wa corona jijini Mwanza.

Barakoa hizo ambazo zimetolewa kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Idadi ya ya Watu (UNFPA), kupitia Taasisi ya Benjamini Mkapa zilikabidhiwa mwishoni mwa wiki jijini Mwanza na Ofisa Miradi wa taasisi hiyo Kanda ya Ziwa, Emmanuel Mashana.

Taasisi zilizonufaika na msaada huo ni Hospitali ya Wilaya ya Nyamagana, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na Kituo cha Afya cha Mamlaka ya Bandari jijini Mwanza.

Mratibu huyo alisema wamepokea na kugawa boksi 1,032 kwa Ilemela, Nyamagana boksi 1,056 na bandari boksi 56.

Mashana alisema msaada huo utasaidia mapambano ya ugonjwa wa corona, ambao umezidi kushika kasi katika mikoa mbalimbali ikiwamo ya Kanda ya Ziwa.

Alisema baada ya msaada huo, wanatarajia kupokea 'gloves' za kuvaa mikononi zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 53 ambazo pia watazigawa katika maeneo ya Kanda ya Ziwa.

Aliongeza kuwa mikoa yote ya kanda hiyo itanufaika na barakoa hizo pamoja na baadhi ya wilaya na maeneo ambayo yapo mipakani.

Akipokea msaada huo, Mratibu wa Kituo cha Afya cha Mamlaka ya Bandari jijini Mwanza, Bernald Moshi, aliishukuru taasisi hiyo.

Alisema barakoa hizo zitawasaidia kujikinga na ugonjwa wa corona ambao umeenea katika maeneo mbalimbali katika Kanda ya Ziwa.

# Mghwira kuzikwa mkoani Arusha leo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

ALIYEWAHI kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, anatarajiwa kuzikwa leo nyumbani kwake, Makumira wilayani Arumeru mkoani hapo.

Kwa mujibu wa msemaji wa familia ambaye ni mdogo wa marehemu, Helen Mghwira, wanasubiri mtoto mkubwa wa marehemu, Fadhili Mgwira, ambaye anafanya kazi nchini Uingereza.

"Dada yetu Anna tutamzika hapa hapa nyumbani kwake Makumira na kwa sasa tunaendelea na taratibu za maandalizi wakati tukimsubiri mtoto mkubwa wa marehemu Wakili Fadhili," alisema.

Alisema familia imepata pigo kubwa la kuondokewa na mwanafamilia ambaye alikuwa na upendo wa dhati kwa wanafamilia aliyetaka kuona watoto wa jamii inayomzunguka anapata elimu haswa kwa watoto wa kike.

"Dada alikuwa mchapa kazi mwenye moyo wa upendo na kutaka kuona kila mtoto kwenye jamii inayomzunguka anapata elimu kwa wakati," alisema.

Alisema licha ya upendo wake huo, marehemu alikuwa ni mtu wa msimamo ambaye alikuwa akiamua jambo lake ameamua na ni lazima alisimamie litekelezeke.

Kuhusu kifo cha Anna, alisema kimekuwa cha ghafla kwa sababu ameugua muda mfupi lakini hakuwa amezidiwa kiasi cha kupoteza maisha.

Alisema marehemu alianza kuugua Jumatano ya wiki iliyopita ambapo walimpeleka Hospitali ya Nkaoaranga inayomilikiwa na Kanisa la Kinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Meru na kupatiwa matibabu ya kwenda na kurudi nyumbani.

Alisema Jumamosi hali yake ilibadilika na kupeleka Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mount Meru, ambapo alifanyiwa vipimo na kubainika kwamba alikuwa na anasumbuliwa na limonia kali.


IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
AT KISUTU

~~RM~~/CIVIL/~~MISC~~/~~PRO~~/EMPL/~~MATR~~ CASE No. 96 OF 2018

THE CONTRACTORS REGISTRATION BOARD ..........PLAINTIFF

Versus

M/S RANKY INFRASTRUCTURE & ENGINEERING LTD. ..........DEFENDANT

NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION/JUDGMENT/RULING

TAKE NOTICE that, the above mentioned case has been fixed for ~~hearing~~/~~mention~~/judgment/~~ruling~~ on the 10th day of AUGUST 2021 At 7.00 PM

YOU are required to appear in this Court without fail and must produce on that day all the documents upon which you intend to relay in support of your case.

GIVEN under my HAND and the SEAL of the Court this 13th day of JULY 2021.

PRINCIPAL/SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KISUTU – D'SALAAM

TO BE SERVED UPON:

MANAGING DIRECTOR
M/S RANKY INFRASTRUCTURE
& ENGINEERING LTD
P.O. BOX 46006
DAR-ES-SALAAM

216365602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bodi ya Ligi, TFF jipangeni kwa msimu mpya 2021-2022

**MSIMU** wa soka Ligi Kuu Tanzania Bara umemalizika, huku sasa timu zikipambana kwenye usajili wa wachezaji wapya kwa ajili ya msimamo ujao.

Jumla ya timu nne zimeshuka daraja msimu huu, ambazo ni Mwadui, JKT Tanzania, Gwambina FC na Ihefu FC.

Wao Coastal Union na Mtibwa Sugar zimenusurika baada ya kucheza kwenye hatua ya mchujo na zimebaki kwenye Ligi Kuu tayari kwa kuanza msimu ujao.

Ikimbukwe kuwa msimu unaokuja kutakuwa na timu 16 zitakazoshiriki Ligi Kuu badala ya 18 ambazo zilikuwapo kwenye msimu uliomalizika 2020-2021.

Ligi imemalizika, sasa ni wakati wa waendeshaji wa ligi hiyo, ikiwamo Bodi ya Ligi pamoja na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kufanyia kazi changamoto zote zilizojitokeza wakati wa msimu mzima wa ligi hiyo.

Changamoto ni nyingi, zikiwamo mabadiliko ya ratiba ya mechi, wakati mwingine bila kufuata kanuni na taratibu, timu kulalamikia waamuzi kuchezesha kwa upendeleo pamoja na mambo mengine.

Nipashe inatumaini kwamba, vyombo hivyo viwili vinavyohusika na uendeshaji wa ligi vitakaa chini na kufanya tathmini ili kujua nini kifanyike kuhakikisha msimu ujao wa ligi unakuwa bora zaidi kuanzia viwango vya timu, waamuzi kutenda haki katika maamuzi hao na kutobadili badili ratiba ya mechi bila sababu za msingi.

Bila ya kuendesha ligi vizuri, hakuna ubishi kuwa timu zetu hazitacheza kwa kiwango, kwani baadhi yao watakuwa wakishinda bila ya kuwa na uwezo wowote.

Kwa upande wa timu, zile zilizobahatika kuendelea kuwapo zinatakiwa zijipange vizuri ili kuleta ushindani msimu ujao na kuepuka kutumia nguvu nyingi ya kubaki ligi inapofikia ukingoni.

Msimu ujao utakuwa mzuri zaidi kwa timu, kwani timu zitafaidiza zaidi baada ya Azam kuongeza fungu la udhamini wa haki ya matangazo, ambayo timu itapata fedha nyingi zaidi ya msimu unaomalizika.

Yote na yote, kikubwa na muhimu msimu ujao unatakiwa kuendeshwa kwa uhakika tena kwa kufuata kanuni na sheria zilizowekwa ili kuhakikisha kila muhusika anafuata taratibu.

Kama kuna kanuni inatoa mwanya kwa timu kufanya uzembe, basi kanuni hiyo ibadilishwe mara moja ili kuhakikisha kuna kuwa na kanuni kali, ambazo zitazifanya timu kutofanya uzembe.

Pia ziangaliwe sheria au kanuni zinazozibana timu bila sababu za msingi, hizo ziondolewe mara moja au zirekebishwe kwa manufaa ya soka la Tanzania, ambalo kwa miaka mingi liko nyuma kimaendelea.

Siku zote ligi bora hutoa washindi bora na pia hutoa timu bora ya taifa, ambayo hufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa, lakini ligi dhaifu huwa inazaa timu dhaifu ya taifa.

Hivyo, Nipashe tunaamini kwamba, msimu ujao utakuwa na ligi bora zaidi kuanzia kwenye uendeshaji hadi dimbani, kwani utakuwa wakati wa kusahihisha makosa yaliyopita.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ukishangaa ya Mtibwa, utayaona ya Coastal

Na Adam Fungamwango

**NILIBAKI** nashangaa peke yangu kuwaona mamia ya mashabiki wa Coastal Union wakifurahi, kuserebuka na kucheza ngoma baada ya timu yao kufanikiwa kubaki Ligi Kuu.

Hiyo ni Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Mkwakwani waliochapa Pamba ya Mwanza mabao 3-1. Coastal Union ikafanikiwa kubaki Ligi Kuu kwa jumla ya mabao 5-3 kwani kwenye mechi ya awali ililazimisha sare ugenini kwenye Uwanja wa Nyamagana ya mabao 2-2 kwenye mechi za mchujo maarufu kama 'play off'.

Ilikuwa kama vile Coastal Union imetwaa ubingwa wa Tanzania Bara. Mtu ambaye alikuwa haelewi lolote au kutoka nje kama angeona jinsi umati wa mashabiki wa Coastal Union walivyovamia uwanja baada ya mechi kumalizika, na jinsi sherehe zilivyokuwa, wakiwamo hata baadhi ya viongozi wa kitaifa, anaweza kudhani timu hiyo imetwaa ubingwa wa Tanzania au FA Cup, au hata Kombe la Kagame.

Sina maana kuwa hawakutakiwa washangilie, la hasha, lakini kwa klabu kubwa kama Coastal Union ambao ni Mabingwa wa Tanzania Bara mwaka 1988, hawakulazimika kufanya hivyo.

Nionavyo mimi Coastal si timu ya kushangilia kubaki Ligi Kuu. Ni kwa sababu haikupaswa kabisa kuwa huko. Ni timu ambayo ina uwezo kabisa wa kupigania kutwaa ubingwa, au kucheza hata fainali ya Kombe la FA ikitaka.

Coastal Union na Mtibwa Sugar zina ugonjwa unaofanana, lakini sababu za ugonjwa ni tofauti.

Mtibwa nayo imeponea chupuchupu kushuka, ilishinda mabao 4-1 Jumatano iliyopita ikiwa ugenini kwenye mechi iliyochezwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, kabla ya kuchapwa bao 1-0 ikiwa nyumbani, Uwanja wa Jamhuri Morogoro.

Kwa maana hiyo Mtibwa imebaki kwa kushinda jumla ya bao 4-2. Mtibwa nao ni Mabingwa wa Tanzania Bara mara mbili mfululizo mwaka 1999 na 2000.

Ukishangaa ya Coastal Union, utayaona ya Mtibwa Sugar. Kwa nini timu hizi kubwa na maarufu nchini zimefikia hadi kucheza mechi za mchujo?

Tukianza na Mtibwa ni kwamba haiendi na wakati. Inaishi zama zile zile za kutegemea vipaji vya wachezaji wake kutoka kikosi chake cha pili. Haisajili wachezaji wengine. Sana sana itarudisha tu wachezaji wake waliocheza zamani.

Wakati yenyewe ikifanya hivyo, kuna timu ambazo zinapanda tu Ligi Kuu, lakini zinatoa pesa na kusajili wachezaji wa maana, ikiwamo wa kigeni.

Mtibwa kwa sasa imeshindwa kupambana hata na timu za Dodoma Jiji, KMC, Namungo, Biashara United ambazo zimewekeza kwa kusajili wachezaji wenye uwezo ndani na nje ya nchi, yenye ikidhani chipukizi wake waliochanganyika na veterani, wanaweza kuitawala tena ligi kama wakati ule, ambapo Simba na Yanga zilikuwa hazijawekeza kwa wachezaji wengi wa kimataifa.

Ndiyo maana kwa miaka hii miwili mitatu, Mtibwa imekuwa kwenye hali ngumu. Hata msimu uliopita, mechi ya mwisho dhidi ya Ruvu Shooting ndiyo iliyoiokoa isishuke au kwenda 'play off', lakini haikujifunza.

Tukirudi kwa Coastal Union ndiyo kabisa. Ule umati wa mashabiki wake waliojazana haijawahi kutokea kwenye mechi yoyote ya Coastal Union ikicheza na timu yoyote ya Ligi Kuu, ukiondoa ikicheza na Simba au Yanga.

Kuelekea kwenye mechi ile, kuchezwa mpaka kumalizika, Wanatanga walionyesha ushirikiano wa hali ya juu mpaka wakafanikiwa kuibakisha.

Sasa unashangaa, ushirikiano huo siku zote unakuwa wapi? Hivi Coastal ikipata kampani kama ile tangu kuanza kwa ligi hadi mwisho kweli si kila timu ya Ligi Kuu ikienda Tanga itakuwa inaona kama vile inakwenda jehanamu?

Na hii si mara ya kwanza wala ya pili kwa mashabiki wa soka mkoani Tanga kufanya hivyo. Wao wanatumia nguvu kubwa kuzipandisha timu zao. Lakini zinapokuwa zipo Ligi Kuu wanaziacha tu. Yaani wanazichukulia poa. Mambo yanapokuwa magumu sasa, ziko hoi, zinataka kushuka, hapo wanarejea tena na kutoa sapoti yao hadi lao linafanikiwa kama walivyofanya kwenye mechi ya 'play off' dhidi ya Pamba.

Nadhani hili lililotokea ni somo kwa Coastal Union na Mtibwa Sugar. Kinachotakiwa ni kufanyia kazi upungufu wote uliyoonekana ili msimu ujao ukiisha isije ikatokea kama ilivyotokea msimu huu uliomalizika.

## HABARI KITAIFA

# Waziri ashtukia upigaji wa mamilioni jengo la maabara

**Na Thobias Mwanakatwe**

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, ameshtukia ufisadi wa Sh. milioni 72 za ujenzi wa maabara zilizotafunwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita, lakini ujenzi wa jengo hilo haujakamilika kwa zaidi ya miaka 10.

Kutokamilika kwa maabara hiyo kulibainika baada ya Silinde akiwa ameambatana na Mbunge wa Geita Vijijini, Joseph Msukuma, na Mkuu wa Wilaya ya Geita kufanya ukaguzi wa miradi iliyojengwa ambayo kampuni ya GGM ilichangia fedha, lakini haijakamilika tangu mwaka 2012, hivyo kubaki kama magofu.

Silinde alisema inashangaza katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya ripoti inaonyesha ujenzi wa maabara umegharimu Sh. milioni 86 na umekamilika na fedha zimekwisha kumbe ni uwongo, na kwamba serikali haitavumilia uhuni huu.

"Kama kuna watumishi wa umma wamehusika kula hizi fedha kwa kinjama watazirudisha, kazi za serikali haziwezi kudharauliwa kiasi hiki," alisema.

Silinde aliwaagiza viongozi wa Wilaya ya Geita kuiandikia barua kampuni ya GGM wafike kuangalia hatua jengo lilipofikia.

"Waandikiwe GGM barua ndani ya siku tatu watoe maelezo yatakayoambatana na kuja kukagua, na taarifa hizo zikabidhiwe kwa Katibu Mkuu TAMISEMI, Waziri TAMISEMI na mimi Naibu Waziri," alisema.

Silinde alisema taarifa hiyo itakayoandikwa itoe mchanganuo wa gharama zilizotumika katika ujenzi wa maabara, kilichokwamisha ujenzi usikamilike kwa muda mrefu, mchango wa wananchi na halmashauri.

Awali, Musukuma alisema ujenzi wa maabara nyingi katika halmashauri hiyo zimejengwa chini ya kiwango na hazijakamilika, lakini taarifa iliyopo ofisini kwa Mkuu wa Wilaya jengo hilo lilitakiwa likamilike kwa Sh. milioni 86. Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Edith Mpinzile, alisema ujenzi ulipofikia zimetumika Sh. milioni 72, na kwamba mchango wa wananchi ni shilingi 4,510,000.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara, Sabasaba Moshingi, akimkabidhi Mkuu wa Gereza la Masasi mabati 200 yenye thamani ya Sh. milioni 7.8 mwishoni mwa wiki. Katikati ni Mbunge wa Masasi na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji, Geofry Mwambe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mradi wa kila kata kituo cha afya waanza Buchosa

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Buchosa mkoani Mwanza imeanzisha mradi wa ujenzi wa kituo cha afya kila kata ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, kusaidia utoaji wa elimu ya uzazi pamoja na kusogeza huduma ya afya kwa wananchi.

Akizungumza na wananchi wa Kata ya Nyanzenda katika Jimbo la Buchosa kwenye mkutano wa hadhara ambao ulilenga pia kusikiliza kero za wananchi, mbunge wa jimbo hilo, Eric Shigongo, alisema serikali imedhamiria kupunguza au kumaliza kabisa vifo vitokanavyo na uzazi.

Alisema serikali ya awamu ya sita imetoa zaidi ya Sh. milioni 750 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya viwili vya kata za Maisome na Nyanzenda.

Alisema vituo hivyo vikikamilika jimbo hilo litakuwa na vituo vya afya saba na hospitali moja katika jimbo zima.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Buchosa, Maria Kapinga, alisema kuna vituo vya afya 5 vinavyohudumia wananchi, hospitali moja ya halmashauri pamoja na zahanati zipatazo 27.

Mmoja wananchi wa Kata ya Nyanzenda, Anamalia Samsoni, alisema wanakosa elimu ya afya ya uzazi hususani matumizi ya uzazi wa mpango, na kwamba vituo hivyo vikikamilika vitamaliza tatizo hilo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Buchosa, Idama Kibanzi, ambaye ni diwani wa Nyanzenda, alisema kutokana na ukubwa wa kata hiyo, kituo cha afya kitawasaidia wananchi wa kata hiyo.


**CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA**
**S. L. P.** 35928, **DAR ES SALAAM, TANZANIA**
**Simu:** +255 22 2401581, **Nukushi:** +255 22 2401582
**Barua Pepe:** thtuhq@thtu.or.tz **Tovuti:** www.thtu.or.tz

**Tarehe: 26/07/2021**

## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mwenyekiti THTU Taifa anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ya kazi kama ifuatavyo;-

**1.0 CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU ZA JUU TANZANIA (THTU)**

Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya juu Tanzania (THTU) ni miongoni mwa vyama vya wafanyakazi vilivyopo nchini kikiwa kimepata usajili Na. 23 mnamo tarehe 12/12/2008. Kwa mujibu wa katiba yetu, THTU inajumuisha wafanyakazi wa vyuo vikuu, Vyuo vikuu vishiriki (Umma na Binafsi) na Taasisi za Elimu ya Juu zisizo Vyuo Vikuu, Pamoja na mamlaka zinazofuatilia ubora na maendeleo ya elimu nchini Tanzania.

**2.0 KATIBU MKUU – NAFASI 1**

**2.1 Sifa za Mwombaji**

i. Mwombaji anatakiwa awe na shahada ya Uzamili (Master Degree) au Stashahada ya Uzamili (Postgraduate Diploma) katika moja ya fani zifuatazo; Law (Sheria), Mediation and Arbitration (Usuluhishi na Uamuzi), industrial/Labour Relations (Mahusiano Kazini), Development Studies (Taaluma za maendeleo), Human Resource Management (Menejimenti ya Rasilimali watu) au sifa linganifu kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
ii. Awe mwenye Shahada ya kwanza katika moja ya fani zifuatazo; Industrial/Labour Relations (Mahusiano Kazini), Law (Sheria), Development Studies (Taaluma za maendeleo), Human Resource Management (Menejimenti ya Rasilimali watu) au sifa linganifu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
iii. Awe na uzoefu wa kazi katika ngazi ya Menejimenti ya vyama vya
iv. Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta vizuri.

**3.0 KAZI NA MAJUKUMU:**

i. Atakuwa Mtendaji Mkuu wa Chama katika masuala yote yahusuyo Chama;
ii. Atasimamia masuala yote ya nidhamu za watumishi walio chini yake;
iii. Ataandaa na kusimamia ya bajeti ya Chama; iv. Atasimamia mapato na matumizi ya Chama; v. Atakuwa Katibu wa Vikao vyote vya Chama;
vi. Atandaa taarifa kila robo mwaka ya utekelezaji wa shughuli zote za Chama;
vii. Atakuwa Msimamizi wa rasilimali za Chama;
viii. Atakuwa Msimamizi Mkuu wa masuala ya kiutawala na uratibu wa shughuli za Chama;
ix. Atasimamia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Chama;
x. Atafanya shughuli za utetezi wa haki na maslahi ya wanachama/wafanyakazi kwa mujibu wa Katiba ya Chama;
xi. Atatunza kumbukumbu zote za Chama;
xii. Atafanya kazi zozote atakazopangiwa na Mwajiri wake.

**4.0 NGAZI YA MSHAHARA NA MUDA WA AJIRA**

Mshahara utakuwa kwa mujibu wa muundo wa utumishi wa THTU. Hali kadhalika, ajira itakuwa ya mkataba wa miaka mitano (5) na marejeo ya kipindi cha miaka mitano mingine endapo utendaji wake utaridhisha.

**5.0 MASHARTI YA JUMLA**

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 50. ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
v. Picha moja "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
vi. "Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", Hati Matokeo za Kidato cha Nne na Sita, yaani FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS HAVITAKUBALIWA.
vii. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 23 Agosti, 2021 saa 10:00 jioni. viii. Maombi yanaweza kuandikwa kwa Lugha ya Kiswahili fasaha au Kiingereza fasaha na yatumwe kupitia barua pepe (email) ifuatayo: Barua Pepe: **mwenyekiti@thtu.or.tz**

**IMETOLEWA NA:**

**Dkt. Paul L. Loisulie**
**Mwenyekiti THTU Taifa**

216372602

# Masauni aipa TADB majukumu kilimo, uvuvi

**Na Peter Haule**

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, ameiagiza Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kuhakikisha inasaidia kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano hususani katika kukuza sekta za kilimo, mifugo na uvuvi.

Mhandisi Masauni ametoa agizo hilo jijini Dar es Salaam alipotembelea Benki ya TADB ambapo alikutana na kufanya mazungumzo na Menejimenti ya Benki hiyo, katika mwendelezo wa ziara yake ya kutembelea taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, jijini Dar es Salaam.

Mhandisi Masauni alisema kuwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, sekta ya kilimo ni ya kipaumbele kwa kuwa inaenda kuchochea maendeleo ya viwanda ambavyo vingi vinategemea malighafi ya kilimo, mifugo na uvuvi.

"Nataka benki hii ipime mafanikio yake katika kuinua mazao ya kimkakati ambayo yameainishwa ikiwa ni pamoja na zao la kahawa, chai, korosho, pamba, michikichi, alizeti na mengineyo, ambayo ni muhimu katika mipango ya serikali na kukuza uchumi wa nchi," alieleza Mhandisi Masauni.

Alisema kuwa Benki ya TADB inajukumu la kuhakikisha inasaidia wakulima nchini katika mazao ya kimkakati bali pia kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao hayo na masoko.

Mhandisi Masauni alisema katika sekta ya kilimo yapo maeneo ambayo yanapaswa kufanyiwa kazi kwa kiasi kikubwa ili kuleta tija kwa nchi ikiwa ni pamoja na eneo la umwagiliaji, upatikanaji wa mbegu bora na ugani.

Pia alisema kuwa ni lazima benki hiyo iibue fursa za maendeleo kwa kushirikisha taasisi zingine, kama Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na Jumuiya za Wafanyabiashara Tanzania, kwa kuwa kuna wanaoweza kuja na fedha za uwekezaji nchini lakini hawazijui fursa zilizopo katika Sekta ya Kilimo.

Aliipongeza benki hiyo kwa kuwa na maono ya kuwa chombo cha mapinduzi ya sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi na pia kuendelea na kukuza mtaji ambapo wakati wa kuanzishwa kwake benki hiyo ilikuwa na mtaji wa Sh. bilioni 50 hadi kufikia Sh. bilioni 80 kwa sasa.

Alisema licha ya ukuaji wa mtaji huo bado hautoshelezi katika utekelezaji wa mikakati ya benki kwa kuwa uhitaji ni takribani Sh. bilioni 800, hivyo ameitaka benki hiyo kupeleka mapendekezo ya namna ya kukuza mtaji na serikali inavyoweza kusaidia, ili benki hiyo iweze kuwa tegemeo katika kukuza uchumi wa nchi kwa kuchangia uwekezaji katika sekta hiyo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya TADB, Japhet Justine, alisema kuwa mwaka 2018 walitoa mikopo ya Sh. bilioni 33, lakini hadi Julai mwaka 2021 wametoa mikopo zaidi ya bilioni 340, hivyo kuendelea kutimiza nia ya kuwagusa wananchi kwa nguvu zaidi katika sekta mbalimbali za maendeleo.

Alimshukuru Naibu Waziri huyo kwa kufanya ziara katika taasisi yake na kuibua changamoto za kuhakikisha wanafungua fursa kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuangalia unafuu wa riba ili kuwasaidia wakulima na wafanyabiashara, na aliahidi kufanyia kazi maagizo yote yaliyotolewa.



Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Lindi, Maimuna Pathan (kushoto), akipokea zawadi ya kuku kwa Diwani wa Kata ya Nangano, Abdallah Malombe, mwishoni mwa wiki, alipokuwa katika ziara ya kikazi wilayani Liwale, pia alifika Shule ya Sekondari Nangano, na kuahidi kuchangia mifuko 50 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa bweni na taulo za kike kwa wanafunzi wa shule hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wachimbaji wadogo wapewa leseni

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

SERIKALI mkoani Shinyanga, imekabidhi leseni za uchimbaji madini kwa wachimbaji wadogo, katika mgodi wa Nyaligongo uliopo Mwakitolyo wilayani Shinyanga.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemoni Sengati, alikabidhi leseni hizo juzi kwa wachimbaji wadogo kwa vikundi tisa ili kuendelea kuchimba madini bila ya kusumbuliwa.

Dk. Sengati akizungumza na wachimbaji wadogo, aliwahakikishia serikali itaendelea kuwaunga mkono wachimbaji wadogo, na kuwataka waendelee kujiunga kwenye vikundi, ili wapatiwe lesseni za uchimbaji madini na kuwa huru na shughuli zao.

"Kwenye mgodi huu kulikuwa na mgogoro kati ya wachimbaji wadogo na mwekezaji, lakini serikali tumeumaliza, na sasa tunakabidhi leseni rasmi za uchimbaji madini na kazi hii itakuwa endelevu," alisema Dk. Sengati. Naye Mwenyekiti wa Kikundi cha Wachimbaji Wadogo, Amrisaid Mled, alisema kupata leseni hizo kutawasaidia sana katika shughuli zao za uchimbaji madini pamoja na kulipa mapato ya serikali bila ya ukwepaji.

# WAVIU watakiwa kukata bima ya afya

**Na Augusta Njoji**

MKURUGENZI Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko, amewahimiza watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (WAVIU), kukata bima ya afya ili kuwa na uhakika wa kupata matibabu.

Aidha, amelitaka Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na VVU na Ukimwi (NACOPHA), kuimarisha ushirikiano na mitandao ya WAVIU ili kurahisisha uratibu na mgawanyo wa rasilimali kwa walengwa.

Dk. Maboko aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipotembelea ofisi za NACOPHA ikiwa ni sehemu yake ya uratibu na utekelezaji wa majukumu ya tume.

Alisema ni haki ya kila Mtanzania kuwa na bima ya afya na hivyo kupunguza kero za kupata matibabu au WAVIU kuhofia kwenda hospitali kupata huduma kutokana na gharama za matibabu.

Aidha, alisema WAVIU wamekuwa na mitandao mingi ambayo kila mmoja anahitaji kufanya kazi na TACAIDS moja kwa moja jambo ambalo haliwezi kuleta utekelezaji wenye ufanisi.

"NACOPHA ipo hapa kwa ajili ya kuwaunganisha WAVIU wote nchini na kama kuna fursa yoyote inakuwa rahisi kwa walengwa kunufaika kwa kuwa NACOPHA itakuwa inaelewa mtandao upi unafanya nini, sitaki kuona migawanyiko," alisema.

Aliitaka NACOPHA ifanye kazi inayofikia malengo ya uanzishwaji wake, ikiwezekana kuwe na idara na vitengo au dawati ili kufikia walengwa wote.

Mbali na hilo, aliwataka WAVIU kuendelea kujiunga katika vikundi vilivyopo katika halmashauri zao, ili kurahisisha upatikanaji wa fedha za mikopo zinazotolewa na serikali.

"Fedha hizi ni kwa ajili ya Watanzania sio vyema kusubiri hadi litengwe fungu la WAVIU, huu mgawanyo uliopo unatosha kwani hata WAVIU wapo katika makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, kwa kutaka mgawanyo maalum wa WAVIU ni kuendeleza unyanyapaa," alisema.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa NACOPHA, Deogratius Rutatwa, alimshukuru Dk. Maboko kwa ushirikiano na usimamizi anaoutoa kwa NACOPHA katika kuhakikisha majukumu yanatekelezeka kwa ufanisi.

"Pia tunashukuru TACAIDS kwa wazo la kuanzisha NACOPHA ambayo leo hii ndio chombo kikubwa cha kuratibu WAVIU wote, naahidi kutekeleza ushauri ulioutoa kwa kuwa ulilenga kuboresha utekelezaji wa majukumu ya NACOPHA," alisema.

Awali, Mwenyekiti wa Taifa wa watu wanaoishi na VVU, Leticia Kapela, alisema NACOPHA ni jukwaa la uratibu, utetezi na uraghibishi wa juhudi zote za WAVIU katika mwitikio wa UKIMWI.

Alisema kwa mujibu wa utafiti bado kuna haja ya kuendelea kuhamasisha wanaume kupima afya zao, ili kujua hali ya maambukizi kwa kuwa mwitikio wao wa kupima unadorora.

# Wachimbaji wadogo kukopeshwa bil. 120/

**Mwandishi Wetu**

WACHIMBAJI wadogo wamepata fursa baada ya Benki ya NMB Plc kusema imepanga kutumia zaidi ya Sh. bilioni 120 kutoa mikopo ya mitaji, vifaa na mitambo kwa wachimbaji wa madini.

Lengo la mpango huo ni kuunga mkono juhudi za serikali za kuongeza tija katika sekta ya madini nchini.

Akizungumza jijini Mwanza wakati wa uzinduzi wa Klabu la Wachimba Madini Kanda ya Ziwa, Mkuu wa Idara ya Biashara kutoka makao makuu ya benki hiyo, Alex Mgeni, alisema hadi sasa benki imetoa mikopo yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 6.3 kwa kundi hilo.

"Wachimbaji wadogo watakopeshwa vifaa na mitambo bila kulazimika kuweka dhamana, kwa sababu mitambo na vifaa hivyo ndivyo vitakuwa dhamana yao baada ya kulipa kuanzia asilimia 20 ya thamani ya kifaa au mtambo anaotaka kununua," alisema Mgeni.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo iliyoshirikisha wachimbaji kutoka mikoa ya Mwanza, Mara, Simiyu, Geita, Shinyanga na Kagera, Rais wa Shirikisho la Wachimba Madini Tanzania (FEMATA), John Bina, alisema uamuzi wa Benki ya NMB kuanzisha dirisha la mikopo kwa sekta ya madini siyo tu utaongeza tija, bali pia utakuza uchumi wa wachimbaji na Taifa kwa ujumla.

"Teknolojia na mitaji ni kati ya changamoto sugu katika sekta ya madini, hasa kwa wachimbaji wadogo; benki ya NMB kutoa mikopo kutamaliza tatizo la mitaji na pengine litamaliza pia suala la teknolojia kwa sababu wachimbaji wataweza kuajiri wataalamu na hatimaye kuchimba kwa tija," alisema Bina.

Alizihakikishia taasisi za fedha fursa ya biashara ya mikopo katika sekta ya madini aliyosema yanaongezeka thamani hata katika kipindi hiki dunia inakabiliwa na janga la virusi vya corona.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, aliihakikishia NMB utayari wa serikali wa kushirikiana na taasisi za fedha na wadau wengine kutekeleza sera na mikakati ya kuongeza tija katika sekta ya madini aliyosema imekuwa kwa kasi ndani ya kipindi cha miaka mitano iliyopita.

"Mchango wa sekta ya madini katika pato la Taifa umepanda kutoka asilimia 3.4 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 5.2 mwaka wa fedha wa 2019/20 na inatarajiwa kufika zaidi ya asilimia 10 ifikapo mwaka 2025. Serikali iko tayari kushirikiana na taasisi za fedha kuongeza tija katika sekta ya madini," alisema Gabriel.

Aliwashauri wachimbaji wadogo kuunganisha nguvu kimtaji kumudu siyo tu kufungua migodi ya kati na mikubwa, bali pia kutoa huduma katika migodi mikubwa ya kimataifa kupitia sera ya local content inayoelekeza sehemu ya huduma migodini kutolewa na kampuni za wazawa.




Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Robert Gabriel, akizungumza wakati wa kuzindua Klabu ya Madini ya Kanda ya Ziwa, (kushoto) Mkuu wa Idara ya Biashara NMB, Alex Mgeni, Rais wa Shirikisho la Wachimba Madini, John Bina na Kaimu Meneja wa Kanda ya Ziwa NMB, Dickson Richard. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi wamwomba mbunge taulo za kike

**Na Sabato Kasika,** LIWALE

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari Nangano iliyoko Kata ya Nangano Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, wamemwomba Mbunge wa Viti Maalum mkoani humo, Maimuna Pathan, kuwasaidia taulo za kike, ili waondokane na kero ya kutohudhuria baadhi ya vipindi darasani anapokuwa katika hedhi.

Ombi hilo likitolewa na mwanafunzi Swadifa Nguate kwa niaba ya wenzake katika mkutano wa mbunge huyo uliofanyika shuleni hapo mwishoni mwa wiki kwenye ziara ya kukagua shughuli za maendeleo.

"Sisi wanafunzi wa kike tuna uhaba wa taulo za kike, hali inayosababisha wakati mwingine tukose vipindi vya masomo darasani anapokuwa katika hedhi, tunaomba utusaidie taulo hizo," alisema Swadifa.

Alifafanua kuwa baadhi yao hulazimika kukaa katika mabweni, huku wenzako wakiendelea na vipindi, hivyo wanaomba kusaidiwa, ili waondokane na hali hiyo wanayokumbana nayo kila mwezi na kusababisha wabaki nyuma katika masomo.

Mbunge Maimuna alipokea ombi la wanafunzi hao na kuahidi kuwasaidia taulo hizo kadri inavyowezekana, kwa kuwa suala la hedhi ni endelevu.

"Nitamtuma katibu wangu aje hapa shuleni kuona ukubwa wa tatizo, kisha mwishoni mwa mwezi nitaanza kusaidia kile nitakachoweza ili kupunguza makali ya tatizo la hedhi kwenye masomo," alisema Maimuna.

Mbunge huyo pia alitoa wito kwa wazazi na walezi kufa kila liwezekanalo, ili kuhakikisha watoto wao hawakosi taulo hizo, kwa kuwa zinawafanya wapate hedhi salama.

Aidha, aliahidi kuchangia mifuko 50 ya saruji kwa ya ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kiume katika ili kuwapunguzia kusafiri umbali mrefu kufuata elimu.

Alitoa ahadi hiyo baada ya kusomewa taarifa ya shule na mkuu msaidizi wa shule hiyo, Ayubu Mwaigomole, aliyoelezea mahitaji ya shule ikiwamo ujenzi wa bweni na jiko la chakula.

Diwani wa Kata Nangano Abdallah Malombe, alisema wakulima wa kata hiyo wamekubali kila mmoja kukatwa shilingi 10 kwa kila kilo ya ufuta ili kuchangia ujenzi huo.

# Bil. 48/- kukamilisha ujenzi vyuo vya VETA

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, amesema Sh.bilioni 48.6, zimetengwa na serikali kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyuo 29 vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA).

Kipanga aliyasema hayo alipotembelea ujenzi wa chuo cha VETA Wilaya ya Kwimba mkoani Mwanza kinachotarajiwa kukamilika Septemba 30, mwaka huu ikiwa ni miongoni mwa vyuo hivyo 29.

Alisema fedha za kukamilisha ujenzi wa chuo hicho zimeshatengwa ili kuhakikisha kinamilika kwa wakati uliopangwa na mafunzo yataanza mara baada ya kukamilika kwa ujenzi huo.

Kipanga alisema gharama za ujenzi wa chuo hicho mpaka kukamilika utatumia zaidi ya Sh. bilioni 2.1, na kwamba hadi sasa imeshatumika sh.Bilioni 1.6 huku Sh. milioni 500 iiliyobaki ikiwa imetengwa katika mwaka wa fedha 2021/22 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa chuo hicho.

Kaimu Mkuu wa Chuo cha VETA Kagera, Juliana Magesa, ambaye ndiye Msimamizi Mkuu wa mradi huo, alisema una jumla ya majengo 17 yakiwamo mabweni mawili yatakayokuwa na uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 144, kati yao 80 wa kiume na 64 wa kike.

Magesa alisema hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 62 na inatarajiwa hadi ifikapo Septemba 30 mwaka huu ujenzi huo utakuwa umekamilika ili kutoa fursa kwa vijana wa Wilaya ya Kwimba na maeneo jirani kupata stadi za kazi watakazozitumia kujiajiri na kuajiriwa na hivyo kukuza uchumi wa Wilaya na Taifa kwa ujumla.

# Sensa ya majaribio kufanyika Agosti

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MAJARIBIO kwa ajili ya sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika mwakani, yatafanyika mwezi ujao.

Tanzania inatarajia kufanya sensa ya watu kwa mwaka ujao 2022 ambayo itakuwa ya sita baada ya iliyofanyika 2012.

Kwa sasa zinafanyika kazi mbalimbali za maandalizi katika maeneo tofauti, huku majaribio ya sensa yakitarajiwa kufanyika Agosti kwenye baadhi ya maeneo Kamisaa wa Sensa ya watu na makazi upande wa Zanzibar, Balozi Mohamed Hamza, alisema maandalizi ya kazi ya sensa yanahitaji umakini mkubwa. Alisema kabla ya sensa yanatakiwa kufanyika majaribio mwaka mmoja kabla, hivyo mwezi ujao majaribio yatafanyika katika maeneo ambayo yamepangwa.

Kamisaa wa sensa Tanzania Bara, Spika mstaafu Anna Makinda, alisema Wilaya ya Kibaha ni kati ya maeneo yatakayoshiriki sensa ya majaribio.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Profesa Kitila Mkumbo (wapili kushoto), akipata maelezo ya uzalishaji wa bia kwa Meneja wa Kiwanda cha TBL Plc Dar es Salaam, Patel Kilovele, alipofanya ziara ya kikazi kiwandani hapo, Ilala Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwenge wabaini ubadhirifu mabilioni wilaya 17

**Na Augusta Njoji,** BAHI

MWENGE wa Uhuru 2021, umebaini dosari mbalimbali ikiwamo ubadhirifu wa fedha za umma kwenye miradi 17 yenye thamani ya Sh. bilioni 11.2 katika wilaya 17.

Aidha, hadi sasa miradi 491 yenye thamani ya Sh. bilioni 786.9 imezinduliwa na Mwenge huo kwenye mikoa 15 iliyotembelewa.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Patrobas Katambi, alitoa kauli hiyo kwenye makabidhiano ya Mwenge huo kati ya Mkoa wa Singida na Dodoma yaliyofanyika jana Kijiji cha Nagulo wilayani Bahi. Katambi alisema miradi iliyokaguliwa ni katika sekta ya elimu, afya, maji, mazingira, kilimo, barabara, uvuvi, ufungaji, fedha na TEHAMA.

Alitaja dosari nyingine zilizobainika kwenye ukaguzi huo ni udanganyifu katika miundombinu, miradi kujengwa chini ya kiwango, kukosekana kwa nyaraka za vipimo vya kimaabara na vifaa vya ujenzi, malipo ya fedha za umma yasiyozingatia taratibu za malipo ya fedha za serikali, migogoro kati ya wananchi na wasimamizi wa mradi na wananchi kutopata huduma inayotarajiwa hasa katika miradi ya maji.

Aliwataka Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa ambao maeneo yao yamekutwa na miradi yenye kasoro watekeleze maelekezo yaliyotolewa na Mwenge ili kurekebisha dosari hizo na kuchukua hatua stahiki dhidi ya watendaji wanaohujumu miradi ya serikali kwa kuzingatia sheria na mamlaka waliyonayo kikatiba. "Pia mikoa na wilaya ambazo Mwenge haujapita mjipange vizuri kwa kuwa Mwenge utaendelea kufanya kazi yake kama ilivyoagizwa na serikali na kuheshimu maelekezo yatakayotolewa," alisema.

Hata hivyo, mkimbiza Mwenge kitaifa, Luteni Josephine Mwambasi, alitoa angalizo kwa viongozi kuhakikisha nyaraka za miradi zinakuwapo eneo la mradi, wahusika waliotekeleza miradi husika na wataalamu wa afya.

"Wakati Mwenge ukiendelea na majukumu yake tukumbuke kuzingatia tahadhari zote za ugonjwa wa Corona, watu wavae barakoa, vitakasa mikono viwepo wakati wote na kila mmoja achukue tahadhari," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alisema kwa Dodoma Mwenge huo utatembea kilomita 1,264.2 kwenye wilaya saba ikiwamo Wilaya ya Bahi na kukagua miradi 36 yenye thamani ya Sh. bilioni 41.88.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, alisema kwa Bahi Mwenge huo utatembea kilomita 125 na kukagua miradi mitano yenye thamani ya Sh. bilioni 1.968.

Awali, akitoa taarifa ya Mkoa wa Singida, Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Binilith Mahenge, alisema Mwenge umetembea kilomita 642.3 na kukagua miradi 55 yenye thamani ya Sh. bilioni 8.182.

# Taasisi ya Clinton, TADB kuinua zao la soya

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imeingia katika ushirikiano wa kimkakati na Clinton Development Initiative (CDI), iliyo chini ya Shirika la Clinton Foundation, ili kutoa mikopo hadi Dola 500,000 (Sh. bilioni 1.15) kwa ajili ya kufungua mnyororo wa thamani wa zao la soya mkoani Iringa.

Kutokana na randama ya maelewano iliyosainiwa na mashirika hayo mawili, ushirikiano huo unalenga kuongeza upatikanaji wa mitaji kwa Vyama vya Msingi (AMCOs) 29 na kuwanufaisha wakulima 2,900 walio katika programu maalumu ya CDI ili kuongeza ufanisi katika uzalishaji na upatikanaji wa masoko kwa zao hilo katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia sasa.

"TADB inayo furaha kubwa kuingia katika ushirikiano huu, kwa sababu ni mara yetu ya kwanza kama benki kujihusisha na mradi katika mnyororo wa thamani wa zao la soya. Pia duniani na hapa nchini, kuna ongezeko mkubwa sana la uhitaji wa zao la soya kama nyongeza ya virutubisho katika chakula cha binadamu.

Kuna wakulima na wajasiriamali wadogo na wa kati, hasa wanawake, ambao wanajishughulisha na biashara hii. Pamoja na hayo, kuna uhitaji mkubwa pia wa soya kama kirutubisho katika chakula cha mifugo pia, hususan kuku," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine.

Aliongeza: "Ushirikiano huu hivyo unawezesha kuwa na mfuko maalum wa mtaji kwa ajili ya kusaidia viongozi wa wakulima, benki za kijamii katika vijiji 'VICOBA' na wanachama wa AMCOs ili waweze kupata mbegu kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora zaidi 'na mbegu zilizothibitishwa kuzalisha nafaka za soya. AMCOs hizi pia zitapata mikopo maalum kwa ajili ya kuwawezesha kununua mapema mazao ya soya na kuwaunganisha katika soko la soya baada ya mavuno."

Naye Mkurugenzi Mkazi wa CDI, Monsiapile Kajimbwa, alisema: "Chini ya ushirikiano huu, CDI imechangia rasilimali kwa ajili ya kufanya mafunzo ya kifedha na maendeleo ya kibiashara ya kilimo, ambapo TADB itakopesha Dola 500,000 sawa sawa na Sh. bilioni 1.15, katika hatua tofauti wa muda wa ushirikiano huu."

Kajimbwa aliongeza, ikiwa uwezeshaji huo utawaongezea kipato wazalishaji wadogo wa soya kwa sababu AMCOs zinazoshirikiana na CDI zina nafasi nzuri zaidi kuwahudumia wanachama wao.

"Kwa miaka mingi, tumefanikiwa katika maeneo ya kutoa mikopo ya pembejeo za kilimo na mikopo ya shughuli baada ya mavuno kupitia vyama vya msingi tunazoshirikiana nazo. Hivyo, huu ni muda muafaka wa kupanua ukubwa wa mradi huu hapa mkoani Iringa, alisema.

Meneja wa Umoja wa Ushirika wa Wakulima Iringa (IFCU), Tumaini Lupola, alisema hatua hiyo ni fursa kubwa kwa IFCU katika kusaidia vyama vya msingi kurasimisha uuzaji wa mazao katika masoko, hususan soya kwa ajili ya kuwanufaisha wanachama na wakulima wao.

"Mikopo hii itawanufaisha sana AMCOs katika kufanya ununuzi wa mapema wa zao la soya kutoka kwa wakulima wao, kukusanya na kuwauzia wanunuzi kwa idadi kubwa na viwango bora zaidi kwa namna bora zaidi."

# Mkumbo atangaza neema ya ujio wa kiwanda cha bia

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, ametangaza neema kwa wakazi wa Dodoma na mikoa ya jirani kutokana na ujio wa kiwanda cha bia.

Kiwanda hicho kinatarajiwa kujengwa na Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) jijini hapa. Kutokana na ujio huo, Waziri Mkumbo amewataka wakazi wa Dodoma kuchangamkia fursa kutokana na ajira zitakazotolewa.

Prof. Mkumbo alisema hayo juzi alipofanya ziara katika Kiwanda cha TBL jijini Dar es Salaam kujionea utendaji kazi na changamoto zilizopo.

Alisema ujenzi wa kiwanda hicho ni matokeo ya uboreshaji na uwekaji wa mazingira bora ya uwekezaji nchini ili kuvutia wawekezaji wadogo na wakubwa kutoka sehemu mbalimbali duniani kuwekeza nchini.

Kutokana na ujenzi wa kiwanda hicho unaotarajiwa kuanza Julai, mwakani na kutarajiwa kukamilika mwaka 2023, Prof. Mkumbo aliwataka wakulima wa shayiri nchini kuongeza uzalishaji kwa kuwa soko la uhakika lipo na linazidi kutanuka.

"Nawapongeza TBL kwa nia pamoja na kuanza mchakato wa kufungua kiwanda kingine jijini Dodoma ambacho ujenzi wake utaanza mwezi Julai, 2022 na kukamilika mwaka 2023 na kuanza uzalishaji," alisema.

Pamoja na pongezi hizo, Prof. Mkumbo aliitaka TBL kubadili mtazamo wa kibiashara kwa kuwa na mawazo ya kujipanua kibiashara na kushindana kikanda badala ya kuwaza soko la Tanzania pekee.

Alisema suala la kujipanua kikanda linakwenda sambamba na msisitizo wa serikali kwamba bidhaa zinazozalishwa nchini, ziuzwe nje zikiwa kamili au bidhaa zilizoongezwa thamani na kuacha utamaduni wa kuuza malighafi.

Kuhusu suala la kodi ya bia kushushwa, Waziri Mkumbo alisema punguzo hilo ni kwa zile ambazo zimezalishwa kwa kutumia shayiri ya Tanzania kwa asilimia 100 na si bia zote.

Mkumbo alisema hatua hiyo inalenga katika kuchochea kilimo cha shayiri nchini na kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vya bia nchini katika kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na kuongeza ajira nyingi.

# Nipashe Spotika




USAJILI 10 GHALI ZAIDI MAN UNITED UK. 12-13



# NYOTA WANAOLIPWA MISHAHARA MIKUBWA EPL

**LONDON,** England

HARY Kane ameripotiwa kukubali dili la kulipwa mshahara wa pauni 400,000 kwa wiki na Manchester City baada ya mwenyekiti wa Tottenham Hotspur, Daniel Levy kukubali yaishe na kumruhusu kujiunga na mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England, EPL.

Straika huyo mwenye umri wa miaka 27 kwa mara ya kwanza alidokeza mpango wake wa kutaka kuondoka Spurs Mei, mwaka huu, kabla ya kujiunga na kikosi cha timu ya taifa ya England kwa ajili ya michuano ya Euro 2020.

Ofa ya kwanza ya Man City ya pauni milioni 100 kwa ajili ya kumsajili Kane ilikataliwa na klabu hiyo ya London kaskazini, kwani Levy alitaka mchezaji huyo aende nje ya ligi hiyo.

Wachezaji wenzake na Kane kwenye kikosi cha England waliripotiwa kudai kwamba, mshambuliaji huyo anaweza kukataa kujiunga na kambi ya mazoezi ya maandalizi ya msimu mpya na Tottenham ili kulazimisha kuondoka hapo Etihad.

Na sasa baada ya kushika nafasi ya pili kwenye michuano ya Euro 2020, Kane yupo tayari kujiunga na Man City.

Hata hivyo, kwa mujibu wa The Sun, hakuna haja tena kwa Kane kugomea mazoezi baada ya Tottenham kuamua kulegeza msimamo wao.

Imedaiwa kuwa fowadi huyo sasa anatarajia kukamilisha uhamisho wa kwenda katika kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola ambapo ada yake inatajwa kuwa ni pauni milioni 160.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Levy ameemtaarifu Kane kuhusu kubadilisha kwa msimamo wake na kwamba sasa yupo tayari kumuachia aondoke.

Kane - ambaye alifunga mabao 23 na pasi za mabao 14 kwenye Ligi Kuu ya England msimu uliopita - anatarajia kusaini mkataba wa miaka minne au mitano na mabingwa hao wa EPL.

Mshindi huyo wa kiatu cha dhahabu kwenye michuano ya kombe la Dunia mwaka 2018, anatarajia kwenda kuziba pengo lililoachwa wazi na Sergio Aguero, ambaye alimaliza muda wake wa kukaa hapo kwa muongo mmoja na kujiunga na Barcelona kipindi hiki cha majira ya joto akiwa mchezaji huru.

Ingawa ripoti nyingine zinadai kwamba, taarifa hiyo ni uzushi, na kwamba Spurs haina mpango wa kumuachia nyota huyo, makala haya inaangalia wachezaji 8 ambao wanaolipwa mshahara wa juu za kwenye Ligi Kuu England.

Kama Kane atatua Man City maana yake yeye ndio atakuwa kinara wa wachezaji wanaongoza kwa mshahara mkubwa, lakini ngoja tuwaangalie hawa kwa sasa;

**#8 Edinson Cavani - Manchester United**

Huyu ni mshambuliaji wa Manchester United ambapo mshahara wake wa sasa analipwa pauni 210,000 kwa wiki na ameongeza mkataba wa mwaka mmoja zaidi kuwachezea mashetani wekundu hao.

**#7 Anthony Martial - Manchester United**

Mchezaji wa Manchester United anayecheza nafasi ya ushambuliaji, Martial yeye yupo nafasi ya tisa kwa wale wanaovuta mkwanja mrefu akiwa anachukua nyumbani pauni 250,000 kwa wiki.

**#6Thomas Partey - Arsenal**

Huyu ni kiungo wa kimataifa wa Ghana, Partey ambaye anakipiga pale Arsenal na mshahara wake ni pauni 250,000 kwa wiki.

**#5 Pierre-Emerick Aubameyang - Arsenal**

Mshambuliaji wa Arsenal na timu ya taifa ya Gabon, Aubameyang analipwa kiasi cha pauni 250,000 kwa wiki na washikabunduki hao wa jiji la London.

**#4 Paul Pogba - Manchester United**

Kiungo wa Manchester United, Pogba ambaye inasemekana hana mpango wa kuendelea kuwachezea Mashetani Wekundu hao, analipwa mshahara wa pauni 290,000kwa wiki.

**#3 Raheem Sterling - Manchester City**

Winga wa Manchester City, Sterling ambaye huenda akaondoka klabuni hapo wakati huu wa dirisha la majira yahaya ya joto, analipwa pauni 300,000 kwa wiki.

**#2 Kevin De Bruyne - Manchester City**

Kiungo wa Manchester City, Bruyne ndiye anayeongoza kwa sasa kupokea mshahara mkubwa zaidi akiwa anachukua pauni 350,000 kwa wiki.

**#1 David de Gea - Manchester United**

Golikipa huyu wa Manchester United kwa sasa anachukua nyumbani kiasi cha pauni 375,000 kwa wiki.

## ISIKUPITE

TIMU za Coastal Union na Mtibwa Sugar, zimefanikiwa kubaki Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kupata matokeo mazuri kwenye mechi zao mbili za mchujo dhidi ya Pamba na Transit Camp ambazo zimetoka Ligi daraja la Kwanza. Kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga, Coastal Union iliichapa Pamba kutoka Mwanza mabao 3-1 na kuifanya timu hiyo kushinda jumla ya mabao 5-2, kwani Jumatano iliyopita timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2 kwenye Uwanja wa Nyamagana, Mwanza. Mtibwa nayo imefanikiwa kubaki Ligi Kuu, licha ya kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Transit Camp kwenye Uwanja wa Jamhuri Morogoro, kwani kwenye mechi ya kwanza Uwanja wa Uhuru, Jumatano iliyopita, Mtibwa ilishinda mabao 4-1.



# USAJILI 10 GHALI ZAIDI MAN UNITED



POGBA

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United imekuwa moja ya klabu yenye mafanikio zaidi Uingereza tangu Ligi Kuu ya England ilipoundwa upya mwaka 1992, na hilo limetokana na kuwa na wachezaji wa kiwango bora kabisa waliowahi kucheza hapo.

Klabu kamwe haijawahi kuwa na woga kwenye matumizi ya fedha katika kusajili mchezaji yoyote, na hilo limewasaidia kushinda mataji 13 ya Ligi Kuu pamoja na mengine ya nyumbani na Ulaya.

Huku wakiwa na rekodi nzuri ya kuwakuza wachezaji wao vijana kutoka katika akademi yao na kupandishwa kikosi cha kwanza kama vile Ryan Giggs, Paul Scholes, David Beckham na Marcus Rashford.

Wengine ni wale muhimu ambao wamenunuliwa kwa fedha nyingi na wakafanya makubwa klabuni hapo.

Lakini pamoja na yote usajili gani wa gharama zaidi katika historia ya klabu hiyo?

Soma makala haya uweze kujua;

**#10 Juan Mata - Pauni Mil 37.**1

Baada ya kukosa nafasi kule Chelsea chini ya kocha, Jose Mourinho, Juan Mata alinunuliwa na David Moyes ili kuisaidia kuimarisha kiwango cha United katika msimu wake wa kwanza hapo Old Trafford.

Ameendelea kuwa hapo hadi leo, lakini hajaweza kuonyesha kiwango cha juu kama alivyofanya kule Stamford Bridge. Hajawa na nafasi ya kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara katika kikosi cha kwanza hapo kwa mashetani wekundu na ameongezewa mkataba wa miezi 12.

**#9 Nemanja Matic - Pauni Mil 40**

Mashetani wekundu hao walikuwa na uhitaji mkubwa wa kiungo wa kati mwaka 2017, na Kocha Jose Mourinho akaamua kumsajili Matic kwa pauni milioni 40.

Raia huyo wa Serbia amekuwa na kiwango cha kuvutia tangu alipotua pale Old Trafford na hivi karibuni alisaini mkataba mpya ambao utamweka hapo hadi mwaka 2023.

**#8 Bruno Fernandes - Pauni Mil 47**

Baada ya kumwania kwa miezi kadhaa, Manchester United hatimaye wakafanikiwa kuipata saini ya Bruno Fernandes.

Man United walikamilisha usajili wa nyota huyo wa kimataifa wa Ureno Januari mkwaka 2020.

Tangu kutua kwake hapo Man United, amekuwa na mchango mzuri kwa timu na amekuwa akilinganishwa na gwiji wa zamani wa United, Eric Cantona.

**#7 Fred - Pauni Mil 47**

Alikuwa anawaniwa kwa udi na uvumba na majirani zao Manchester City ili kwenda kuongeza nguvu kwenye kikosi chao.

Lakini Fred mwenyewe akaamua kuichagua Man United iliyokuwa chini ya kocha Jose Mourinho na akajiunga na kikosi hicho mwaka 2018.

Alikuwa na wakati mgumu wa kuzoea mazingira katika mwaka wake wa kwanza na nusu hapo, lakini sasa ni mmoja wa viungo muhimu zaidi kwa kikosi cha kocha, Ole Gunner Solskjaer linapokuja suala la mechi kubwa.

**6. Aaron Wan-Bissaka - Pauni Mil 50**

Baada ya kuonesha kiwango cha kuvutia sana kwa kikosi cha Crystal Palace, huku akionesha uwezo wa hali ya juu, Man United wakalazimika kutumia kiasi cha pauni milioni 50 ili kunasa saini ya mlinzi huyo kijana.

Kiulinzi amekuwa na kiwango kizuri na amekuwa na nafasi ya kucheza mara kwa mara kwenye kikosi hicho na inaonesha wazi kwamba, ana nafasi kubwa ya kuendelea kung'ara zaidi.

**#5 Angel Di Maria - Pauni Mil 59.7**

Baada ya kulazimika kuondoka kule Real Madrid, Di Maria alisajiliwa kwa ada ambayo wakati huo iliweka rekodi ya pauni milioni 60 na akapewa jezi namba saba.

Alianza vizuri, lakini baadaye akajikuta akiwa hana nafasi chini ya kocha, Louis Van Gaal, na haraka akaondoka kipindi cha majira ya joto kilichofuata na kuelekea jijini Paris kujiunga na PSG.

**#4 Jadon Sancho - Pauni Mil 73**

Hili ni dili la hivi karibuni zaidi, Manchester United wamemsajili kijana mwenye kipaji kujiunga na kikosi chao hiyo kwa mkataba wa miaka mitano, akitokea kule kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, katika klabu ya Borussia Dortmund.

Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 21 sasa, ameigharimu kiasi cha pauni milioni 73, na anaonekana atakuwa na wakati bora zaidi katika miaka inayokuja hapo Old Trafford.

**#3 Romelu Lukaku - Pauni Mil 75**

Baada ya kung'ara kule Everton, Manchester United ikalipa pauni milioni 75 ili kumsajili Lukaku hapo Old Trafford wakati kocha Jose Mourinho alipokuwa anaangalia mtu wa kuziba pengo la Zlatan Ibrahimovic.

Lukaku alifunga mabao 27 katika msimu wake wa kwanza, lakini baadaye akawa sio tena chaguo la Mourinho ambaye alifukuzwa na y ye akaenda kujiunga Inter Milan kipindi cha majira ya joto kilichofuata.

**#2 Harry Maguire - Pauni Mil 80**

Kocha Ole Gunnar Solskjaer alifanya maamuzi ya kutaka kumsajili beki, Harry Maguire hapo Old Trafford, na alikuwa tayari kufanya lolote linalowezekana.

Klabu hiyo ikatoa kiasi fedha kilichoweka rekodi ya dunia cha pauni milioni 80 kumsajili mlinzi huyo na tangu hapo amekuwa nahodha wa timu hiyo kwa kipindi cha miaka miwili sasa aliyokaa hapo.

**#1 Paul Pogba - Pauni Mil 89**

Baada ya kuondoka kama mchezaji huru na kujiunga na Juventus, Pogba alirudi tena klabuni hapo kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia kwenye usajili ya pauni milioni 89 mwaka 2016.

Muda wake klabu hapo umekuwa wa kupanda na kushuka kwa kipaji chake, kwani kuna wakati amekuwa na kiwango cha juu akiisaidia timu na wakati mwingine amekuwa katika kiwango kibovu na kutokuwa na msaada kwa timu.

Hivi sasa amekataa kusaini mkataba mpya, huku huu wa sasa unamalizika kipindi cha majira ya joto kinachokuja na huwenda akaondoka akiwa mchezaji huru, kama hatauzwa kipindi hiki cha majira ya joto.

## Nukuu

"Tayari ilikuwa heshima kubwa kucheza hapa kwa miaka sita, klabu imeonyesha heshima kubwa kwangu na nina furaha kubwa kuwa hapa. Naona kama nipo nyumbani kwa mashabiki wanaonizunguka, wachezaji wenzangu na benchi lote la ufundi**." Straika wa Tottenham Hotspur, Son Heung-min.**



"Mimi kazi yangu ni kucheza soka. Na nashukuru nilikuwa na mambo fulani hivi yalikuwa hayajakaa sawa, lakini kwa sasa kila kitu kinakwenda vizuri, hata mimi mwenyewe najiona kuwa niko vizuri. Kiwango changu kimeanza kurudi, kwa hiyo mashabiki watamuona yule Kichuya waliomzoea msimu ujao.**" Mchezaji wa Namungo FC, Shiza Kichuya.**



"Tunakwenda kucheza mechi za kimataifa. Tunakwenda kucheza michuano mikubwa na wachezaji wa viwango vya juu kwa hiyo na sisi lazima tujiimarishe. Lengo letu ni kwenda kwenye michuano hiyo tukiwa na wachezaji wenye viwango vikubwa na wazoefu. Tayari tumepata uzoefu kutoka kwenye Ligi Kuu ya Tanzania, lakini tumejifunza kutoka kwenye timu ambazo zimeshiriki michuano ya kimataifa na kujua nini kinahitajika.**" Katibu Mkuu wa klabu ya Biashara United, Haji Mtete.**






# REKODI 8 KALI SIMBA IKITWAA UBINGWA

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21 ilimalizika rasmi Julai 18 na Simba kukabidhiwa ubingwa wa Tanzania Bara msimu huu.

Timu hiyo yenye maskani yake Msimbazi, siku ya mwisho iliichapa Namungo mabao 4-0 na kumaliza ligi ikiwa na pointi 83, kwa mechi 34 ilizocheza.

Katika mechi hizo ilishinda michezo 26, sare tano na kupoteza michezo mitatu.

Ubingwa huo umeipatia tena nafasi ya kwenda tena kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa msimu ujao, ambapo msimu huu iliishia hatua ya nusu fainali.

Kwenye makala haya, tunaangalia rekodi mbalimbali ambazo Simba imeweka msimu huu kwenye Ligi Kuu.

**#1 Kutwaa mara nne mfululizo**

Simba imetwaa ubingwa mara nne mfululizo baada ya miaka 42 kupita. Mara ya mwisho ilikuwa ni mwaka 1979 ilipotwaa mara nne mfululizo kuanzia mwaka 1976. Timu hiyo pia iliendelea kutwaa ubingwa hata msimu uliofuata wa 1980, kabla ya kunyang'anywa mwaka 1981 na Yanga, hivyo kuweka rekodi ambayo inayo hadi leo ya kutwaa mara tano mfululizo.

**#2 Kufunga mabao mengi**

Imetwaa ubingwa ikiwa imefunga mabao mengi zaidi kuliko timu nyingine yoyote ile. Simba imeweka nyavuni mabao 78 kwenye Ligi Kuu msimu huu, ikifuatiwa kwa mbali na watani zao wa jadi Yanga ambao walifunga mabao 52 tu.

**#3 Imefungwa mabao machache**

Mbali na kutwaa ubingwa, Simba imeweka rekodi nyingine ya kuwa timu iliyofungwa mabao machache zaidi. Imefungwa mabao 14 tu kwa mechi 34 ilizocheza, ikifuatiwa na Yanga ambayo imefungwa mabao 22.

**#4 Straika wake atwaa kiatu**

Rekodi nyingine ambayo imeweka Simba ni kwamba straika wao, John Bocco ametwaa kiatu cha dhahabu. Bocco, aliyesajiliwa na klabu hiyo mwaka 2017, amekuwa mfungaji bora wa msimu baada ya kukwamisha wavuni mabao 16.

**#5 Mastraika wake wafuatana kileleni**

Nusura wachezaji wa timu hiyo wawili, Bocco, na Chriss Mugalu wagongane kwa mabao 15 ambapo ingekuwa ni rekodi ya aina yake, kabla ya Bocco kupata bao kwa mkwaju wa penalti dakika za mwisho kwenye mechi dhidi ya Namungo na kuwa wa 16.

Msimu huu Simba imeweka rekodi ya wao kufuatana kileleni kusaka kiatu cha dhahabu na ilikuwa ni vigumu kutabiri nani angetwaa.

Wachezaji hao ni Bocco aliyemaliza na mabao 16, Mugalu aliyeshika nafasi ya pili kwa mabao 15, pamoja na Meddie Kagere aliyekamata nafasi ya nne kwa mabao 13. Aliyechafua gazeti ni Prince Dube wa Azam FC aliyeshika nafasi ya tatu kwa kumaliza na mabao 14.

**#6 'Kiatu' mara ya nne mfululizo**

Timu hiyo imeweka rekodi nyingine ya mastraika wake kuwa wafungaji bora kwa misimu minne mfululizo.

Tangu msimu wa 2017/18, Simba imekuwa ikitoa mfungaji bora hadi msimu huu.

Msimu wa 2017/18, Mganda Emmanuel Okwi alitwaa kiatu cha dhahabu akipachika mabao 20, na msimu wa 2018/19, Mnyarwanda, Meddie Kagere alikuwa mfungaji bora, akipachika mabao 23, akatetea tena nafasi yake msimu uliofuata wa 2019/20 akikwamisha mabao 22, na msimu huu Bocco ameifanya Simba kutetea tena nafasi hiyo kwa mabao 16.

**#7 Kipa wake aongoza kwa 'clean sheet'**

Kipa wa Simba, Aishi Manula ameiongezea tena timu yake rekodi, kwa kuongoza kucheza mechi nyingi

Manula amemaliza ligi akiwa na 'clean sheet' 18, akifuatiwa na kipa wa Mbeya City Haroun Mandanda ambaye amesimama golini mara 15 bila kuruhusu wavu wake kutikiswa.

Metacha Mnata wa Yanga na Abutwalib Mshery wa Mtibwa Sugar, wana 'clean sheet' 13 kila mmoja, huku Jeremiah Kisubi wa Prisons.

Kipa mkongwe Juma Kaseja yeye amesimama langoni mara 11 bila kuruhusu bao pamoja na Aron Kalambo wa Dodoma Jiji, huku Daniel Mgore wa Biashara United akiwa na 'clean sheet' 10.

**#8 Mastaa wake waliongoza 'assist'**

Kwa mara nyingine tena, Simba imeweka rekodi kwa mchezaji wake Clatous Chama kutoa pasi nyingi za mabao maarufu kama 'assist'.

Hadi Ligi Kuu Tanzania Bara inamalizika, Chama ametoa 'assist' 15, akifuatiwa na mchezaji wengine wa Simba, Luis Miquissone ambaye ametoa pasi za mwisho kumi.

**JE, WAJUA?**



WINGA wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi, amekataa mpango wa kufanywa chambo ya kubadilishwa na nyota wa Bayern Munich, Kingley Coman.





# Benki zaombwa kupunguzia riba wakulima

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Aldolf Mkenda, ameziomba benki kupunguza riba ya mikopo kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji kwenye kilimo cha alizeti.

Prof. Mkenda alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akifunga Wiki ya PASS Trust jijini Dodoma na kuzinduliwa kwa Kampuni ya Leasing ya kukopesha wakulima zana za kilimo bila dhamana na kwa riba nafuu.

Alisema serikali inatumia fedha nyingi kwa ajili ya kuagiza mafuta ya kula nje, hivyo kama wakulima watawezeshwa itasaidia kuongeza uzalishaji wa alizeti na kutosheleza kwenye viwanda.

"Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kwa ajili ya kuagiza mafuta na hii inatokana na viwanda vya alizeti kushindwa kuzalisha mbegu za mafuta kwa wingi ambazo zitasaidia viwanda hivyo kufanya kazi kwa mwaka mzima," alisema Prof. Mkenda.

Aidha, alisema wizara itahakikisha wanapata mbegu bora ambazo wakulima wanaolima kwa mkataba

watapatiwa ili kulima zao hilo kwa wingi.

Pia alisema wizara hiyo imeanzisha operesheni ya miaka mitatu hadi minne yenye mikakati inayotekelezeka kwa ajili ya kukuza kilimo cha alizeti.

"Tumeteua mikoa mitatu ambayo itapewa kipaumbele katika huduma za ugani ili kuwa mstari wa mbele kuzalisha zao la alizeti," alisema.

Alizipongeza Sweden na Denmark kwa kujitokeza kusaidia juhudi za PASS TRUST kuhakikisha inakuwa imara ili kuendelea kutoa mikopo kwa wakulima.

"Nitajipanga kuwaona mabalozi wa nchi hizo ili fedha watakazotoa ziendelee kutumika kwa ajili ya manufaa," alisema Prof. Mkenda.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya PASS TRUST, Anna Shanalingigwa, alisema taasisi hiyo itaendelea kushirikiana na wizara hiyo kwa ajili ya kuinua sekta hiyo nchini kwa kuwa asilimia 60 ya Watanzania wanategemea kilimo.

Shanalingigwa alisema PASS Trust ipo mstari wa mbele kuhakikisha wakulima wananufaika na fursa za mikopo ambazo zinatolewa na taasisi hiyo ili kujiinua kiuchumi.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, aliwataka wakulima kuendelea kufanya kazi na PASS Trust kwa sababu itawasaidia kuwainua kiuchumi kutokana na mikopo ambayo wanatoa kwa wakulima.

Aliwashauri kujipanga kuanzisha mashamba ya zabibu na alizeti kwa kuwa ni mazao yanayostawi latika Mkoa huo na yana manufaa ya kibiashara.



Mbunge wa Kisesa, Luhaga Mpina, akikata utepe kuashiria uzinduzi wa harambee ya ujenzi wa jengo la kituo cha watoto na jengo la kuabudia la Kanisa la Waadventista Wasabato (SDA), Ihumwa jijini Dodoma, kwenye harambee hiyo alichangisha zaidi ya Sh. milioni 31.1.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# EWURA yaja na dawa ya vishoka wa umeme

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetoa leseni 5,865 kwa mafundi wa ufungaji na watandazaji wa nyanya za umeme kwenye nyumba ikiwa ni mikakati ya kudhibiti vishoka.

Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Titus Kaguo, alibainisha hayo jijini hapa kwenye semina iliyotolewa na mamlaka hiyo kwa Taasisi ya Maendeleo ya Viziwi Tanzania (TAWAVITA) alipokuwa akibainisha mafanikio katika sekta ndogo ya umeme hususani kwenye usimamizi wa wafungaji na watandazaji wa nyaya za umeme.

Kaguo alisema EWURA inasimamia mafundi wa kutandaza nyaya za umeme ili kuhakikisha kuwa huduma zao zinafanyiwa kitaalamu na kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu.

"Mpaka sasa zaidi ya mafundi 5,865 wamepewa leseni na EWURA katika madaraja mbalimbali kwa kuzingatia ujuzi na elimu zao. Kwa mwaka 2019/20 pekee, EWURA ilitoa leseni kwa mafundi 963," alisema.

Alisema uwapo wa mafundi wenye leseni umewezesha kupunguza matukio ya ajali za moto kunakosababishwa na ufungaji na utangazaji duni wa nyaya za umeme.

"Naomba mafundi wa umeme hakikisheni mnakuwa na leseni za kazi zinazotolewa na EWURA ili msipishane na fursa mbalimbali," alisema.

Kaguo alitoa rai kwa wananchi kuhakikisha fundi anayetumia kufunga na kutandaza nyaya za umeme kwenye nyumba zao awe na leseni kutoka EWURA.

"Msichukue fundi ili mradi fundi, hakikisha ana leseni kutoka EWURA, hii itakuhakikishia usalama wa mali zako," alisema.

Aidha, Kaguo alisema EWURA pia imeandaa na kuweka taratibu mbalimbali ikiwamo utoaji wa leseni wa haraka ndani ya miezi miwili, kwa uwazi, na ushirikishwaji mpana, uidhinishaji wa mikataba ya kuuziana umeme na uandishwaji wa mkataba wa wateja kwa TANESCO.

Alisema pia EWURA imeandaa kanuni za miradi midogo ya umeme, mikataba maalum ya kuuziana umeme na kanuni za kupanga bei ya umeme ili kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi kwenye miradi midogo ya kuzalisha umeme kwa kutumia nishati jadidifu.

# Sababu waliotoka gerezani kurudia makosa yaanikwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

UNYANYAPAA kwa wafungwa wanaomaliza vifungo na kurejea uraiani umetajwa kuwa ni chanzo cha kufanya makosa tena na kurudi gerezani.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Magereza (SACP), Justine Kaziulaya, aliyasema hayo katika mkutano uliofanyika kwa njia ya mtandao kati ya Tanzania, Israeli, Mauritiusi na Shelisheli.

Alisema suala hilo linasababisha wao kwenda kukaa mbali na familia zao ili kukwepa unyanyapaaji unaofanywa dhidi yao baada ya kutoka gerezani.

"Kutokana na unyanyapaa, wafungwa wengi wanaomaliza vifungo vyao hawajisikii amani kurudi katika jamii zao, hivyo kulazimika kwenda kuishi mbali na nyumbani kwao, hali ambayo wakati fulani huwalazimisha kurudia kufanya makosa na kujikuta wakirudi tena magerezani," alisema.

Alizitaja baadhi ya kero nyingine ni mtazamo finyu wa jamii kuhusu adhabu mbadala, ukosefu wa mitaji na vitendea kazi kwa wafungwa wanaorejea uraiani.

Akihitimisha mawasilisho yake, Kamishna Kaziulaya alisema kuwa suala la kuwapokea tena wafungwa wanaorejea uraiani linahitaji mtazamo wa pamoja na hasa ikizingatiwa kuwa suala la urekebishaji wa tabia zao mtambuka ambalo linatakiwa ushirikishwaji wa jamii nzima.

Katika mkutano huo ulioandaliwa na Idara ya Magereza ya Ushelisheli kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Ushelisheli, washiriki walipata fursa ya kuwasilisha, kujadiliana na kubadilishana uzoefu wa kazi mbalimbali zinazofanywa na Idara ya Magereza katika suala zima la urekebishaji wa wafungwa katika nchi zao.

Mkutano huo ulifanyika katika kumbukizi ya siku ya Rais wa kwanza mzalendo wa Afrika Kusini, Hayati Nelson Mandela, inayoadhimishwa kila mwaka kimataifa ikiwa ni kukumbuka mchango wake kwenye magereza.





Meya wa Jiji la Mbeya, Dour Issa Mohamed (kushoto), akiwa na baadhi ya viongozi wa Bodi ya Shule ya Sekondari Iduda ya jijini humo, kukagua ujenzi wa miundombinu unaoendelea shuleni hapo, hivi karibuni. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# RC aagiza msako wanaodaiwa kuhujumu barabara

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WANANCHI wilayani Chunya, wanadaiwa kuhujumu miundombinu ya barabara ya Chunya-Makongolosi yenye urefu wa kilomita 39 inayojengwa kwa kiwango cha lami kwa kuiba alama za barabarani na kuchimba mchanga kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara hiyo.

Mradi huo unajengwa kwa kutumia fedha za serikali na unatekelezwa na Mkandarasi China Railway 15 Bureau Group Corporation na unatarajiwa kukamilika Agosti 30, mwaka huu.

Akitoa taarifa ya mradi huo juzi wakati Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya ilipofanya ziara ya kukagua mradi huo, mwakilishi wa mkandarasi anayejenga barabara hiyo, Mhandisi Bruno Ruburi alisema wananchi hao wameng'oa baadhi ya alama na kutokomea nazo.

Alisema hujuma hizo zinaweza zikasababisha kuchelewa kukamilika kwa mradi huo na gharama kuongezeka hivyo akaiomba serikali iwasaidie kukabiliana na tatizo hilo ambalo alisema tayari walishatoa taarifa katika kituo cha polisi cha wilaya hiyo.

"Lakini uchimbaji wa mchanga kwenye hifadhi ya barabara unasababisha barabara kuanza kubomoka hata kabla haijakamilika, na sisi lengo letu tunataka ndani ya miezi miwili tukabidhi serikalini," alisema Mhandisi Ruburi.

Baada ya taarifa hiyo Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ambaye aliiongoza Kamati ya Ulinzi na Usalama kukagua miradi wilayani humo aliliagiza Jeshi la Polisi kuwasaka na kuwakamata watu wote wanaofanya hujuma hizo. Alisema wakikamatwa wanatakiwa kuchukuliwa hatua kali za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani kwa madai kuwa fedha zinazotumika kutekeleza mradi huo ni kodi za Watanzania na hivyo serikali haiwezi kuwavumilia.

Alilitaka jeshi hilo kushirikiana na wananchi wa Wilaya ya Chunya kuwafichua wahalifu hao huku akitaka apewe taarifa ndani ya muda mfupi kwamba wahusika wamekamatwa na hatua zimeanza kuchukuliwa dhidi yao.

"Hawa wananchi wanawajua watu hao maana wakiiba huko wanakuja kuuza humuhumu mitaani, wanatengenezea mashoka na zana zingine, mkishirikiana vizuri na hawa wana watawaambia mambo mengi sana kwahiyo nawaachia hiyo kazi lazima ifanyike," aliagiza Homera.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, aliahidi kutoa zawadi nono kwa mwananchi yeyote ambaye atasaidia kuwafichua wahalifu wanaohujumu barabara hiyo huku akisisitiza kuwa siri itafichwa. Aliwataka wananchi wa wilaya hiyo kuilinda miundombinu ya barabara hiyo kwa maelezo kuwa wao ndio wanufaika wa kwanza wa uboreshaji wa barabara hiyo ikiwamo kupungua kwa nauli pamoja na kusafirisha mazao yao bila vikwazo.

"Serikali imetusaidia sana, sasa hivi hapa Makongolosi pamekuwa pazuri kuliko Chunya Mjini, mmewekewa mpaka taa za barabarani ambazo zitawasaidia kufanya kazi zenu kwa raha, sasa nawaombeni mtusaidie kuwabaini wahalifu hawa," alisema Mayeka.

Nao baadhi ya wananchi wa Mji Mdogo wa Makongolosi walisema hujuma hizo zinaweza zikaikatisha tamaa serikali na kusababisha isiwapelekee miradi mingine muhimu na hivyo lazima washiriki kuilinda barabara hiyo.

Amos Sinkonde, alisema mpaka sasa hali ya usafiri katika wilaya hiyo imeanza kuwa nzuri kwa maelezo kuwa kwa sasa wanatumia muda mfupi kutoka Makongolosi kwenda Chunya Mjini, na kwamba wameahidiwa nauli kupungua kutoka Sh. 4,000 ya sasa mpaka Sh. 2,000.

Barabara hiyo ni sehemu ya barabara ya Mbeya-Tabora ambayo serikali iliahidi kuijenga kwa kiwango cha lami kwa hatua ili kuiunganisha mikoa hiyo kwa lami.

# Soko la maziwa lasababisha hasara mabilioni h/shauri 2

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

HALMASHAURI za Rungwe na Busokelo zinapoteza zaidi ya Sh. bilioni 50 kila mwaka kutokana na maziwa ambayo wananchi wanazalisha kukosa soko, hivyo kumwagwa na mengine kuuzwa kwa bei ya hasara.

Aidha, inadaiwa kuwa kukosekana kwa soko la uhakika la maziwa hayo kumesababisha baadhi ya wananchi kuanza kuuza mifugo yao ili wawekeze kwenye shughuli zingine ambazo zinawalipa.

Mbunge wa Busokelo, Atupele Mwakibete, aliyasema hayo wakati wa kikao cha wadau wa maendeleo wa halmashauri zote mbili ambacho kililenga kutatua kero ya kukosekana kwa soko la maziwa. Alisema maziwa hayo yanakosa soko kutokana na wilaya hiyo kutokuwa na viwanda vya kuchakata maziwa, hivyo akashauri watafutwe wawekezaji ambao watawekeza kwenye viwanda vya kuchakata bidhaa zitokanazo na maziwa.

"Baadhi ya wananchi wameanza kukata tamaa ya kuendelea kufuga, sasa ni wajibu wetu kuwatafutia wananchi wetu masoko ya uhakika, hapa tunamtegemea mnunuzi mmoja pekee ambaye yupo Iringa na asiponunua basi wananchi wanamwaga na ndio tunapata hasara," alisema Mwakibete.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, alisema ili kukabiliana na tatizo hilo wanakusudia kuwapa kipaumbele cha mikopo ya halmashauri wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambao wataanzisha viwanda vidogo vya kuchakata maziwa.

Aidha, alisema wadau walikubaliana kujenga viwanda viwili katika wilaya hiyo ambavyo kimoja kitakuwa Busokelo na kingine Rungwe ili visaidie kukabiliana na tatizo la ukosefu wa soko la maziwa kwa wananchi wa Wilaya hiyo.

Vilevile, alisema waliunda kamati maalumu ya kufuatilia na kujua soko la maziwa ili wananchi washauriwe vizuri na kwamba kamati hiyo pia itafanya kazi ya ufuatiliaji wa ujenzi wa viwanda.

"Wananchi wanafanya kazi kubwa na hakuna anayewalazimisha, wanazalisha mazao ya kilimo na wanafuga, lakini tatizo kubwa lililopo ni masoko, sasa hivi mwananchi wa Rungwe akitamani kula 'Yogurt' ni lazima anunuwe za ASAS ambazo zinazalishwa Iringa," alisema Dk. Anney.

Alisema wilaya hiyo inawakaribisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwenda kuwekeza wilayani humo, na kwamba maeneo ya kuwekeza yapo na wataandaa mazingira rafiki ya uwekezaji.

Baadhi ya wafugaji walisema kwa sasa wanamtegemea mwekezaji wa Kampuni ya ASAS ambaye alishapatiwa eneo la kujenga kiwanda kwamba yeye ndiye atakayekuwa mkombozi wao.

Mmoja wa wafugaji hao, Daniel Mwalwayo, alisema ambaye ni mkazi wa Kiwira wilayani Rungwe, alisema asilimia ndogo ya maziwa wanawauzia wapita njia ambao alisema huwa wanauza lita moja kati ya Sh. 1,000 na 1,500.

Alisema bei hizo haziendani na gharama wanazotumia kuitunza mifugo yao na hivyo baadhi yao wanakata tamaa.

## Utendaji wa Dk. Tulia waikosha CCM

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbeya Mjini, kimemkabidhi Mbunge wa Jimbo hilo, Dk. Tulia Ackson, cheti maalumu cha kutambua mchango wake kwa chama hicho pamoja na kuwatumikia wananchi wa Jimbo hilo.

Dk. Tulia alikabidhiwa cheti hicho mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Chama hicho Wilaya ya Mbeya Mjini, Afrey Nsomba katika hafla iliyofanyika ofisi za chama hicho zilizopo katika eneo la Sabasaba jijini hapa.

Nsomba alisema Dk. Tulia amekuwa akitoa michango mbalimbali kwa ajili ya shughuli za chama hicho pamoja na kuchangia miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo inatekelezwa ndani ya wilaya hiyo na kwamba hawajawahi kuwa na mbunge mwenye moyo wa aina hiyo.

"Amechangia ujenzi wa miundombinu ya elimu kwenye shule mbalimbali zilizomo ndani ya jimbo na hata nje, kwenye afya ndio mahali pake, amesaidia kujenga wodi za kinamama kwenye vituo vyetu vya afya," alisema Nsomba.

Alisema kutokana na michango hiyo chama hicho kiliamua kumtunukia cheti kama sehemu ya kuonyesha kuridhishwa na utendaji wake wa kazi na kwamba chama hicho hakina uwezo wa kumlipa.

Alisema kutokana na utendaji huo wana uhakika jimbo hilo ambalo kwa miaka 10 lilikuwa linaongozwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) litaendelea kuwa mali ya CCM kwa miaka mingi ijayo.

Baada ya kupokea cheti hicho Dk. Tulia ambaye ni Naibu Spika wa Bunge, aliushukuru uongozi wa CCM Wilaya ya Mbeya kwa kutambua mchango wake huku akiahidi kuendelea kushirikiana nao kwenye shughuli zingine.

Alisema atahakikisha wananchi wa Jimbo hilo wanapata maendeleo ya uhakika na kwamba Bunge la bajeti lililoisha mwishoni mwa mwezi Juni lilipitisha bajeti ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini ikiwamo katika jimbo hilo.

"Tutahakikisha barabara zetu zinaboreshwa ili wananchi wasipate shida, lakini pia tutashirikiana kumaliza tatizo la maji katika Jiji hili, kama mlivyoona hivi karibuni tulikuwa na Naibu Waziri wa Maji hivi karibuni hapa na alituahidi mambo mengi," alisema Dk. Tulia.

Aliwaomba viongozi wa CCM waendelee kumpatia ushirikiano kwenye usimamizi wa miradi ili itekelezwe kwa viwango vinavyostahili.



## HABARI ZANZIBAR

# SMZ yaona fursa mpya kwa utalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Mohammed Mussa, amesema ujio wa ndege ya Airbus A330-200 kutoka kampuni ya Eurowings Discover ya Ujerumani utachangia kuitangaza Zanzibar kiutalii kama kituo bora cha utalii duniani.

Alikuwa akizungumza jana baada ya mapokezi ya ndege hiyo katika Uwanja wa Abeid Amani Karume (AAKIA) nje ya Mji wa Zanzibar.

Ndege hiyo ambayo iliwasili jana na kupokelewa kwa burudani mbalimbali.

Waziri huyo alisema serikali kupitia wizara itaendelea kutoa ushirikiano na msaada utaohitajika kuhakikisha safari za ndege hiyo inaendelea na kuwa za mafanikio kwa faida ya biashara ya kampuni hiyo na kuimarika kwa uchumi wa Zanzibar, ambao unategemea zaidi sekta ya utalii.

Waziri Lela alilishukuru Shirika la Eurowings Discover pamoja na kundi la Lufthansa kwa maamuzi yao ya kuichagua Zanzibar kuwa moja ya vituo vyao vya safari za moja kwa moja kutoka Ulaya.

Aidha, aliyaaka mashirika mengine ya ndege kufanya safari zake Zanzibar, kwa sababu Zanzibar ipo salama na ina mandhari mazuri pamoja na vivutio vingi vya utalii.

"Nchi za wenzetu wana vizuwizi kutokana na ugonjwa wa corona, sisi Tanzania ikiwamo Zanzibar tupo salama... tunayaomba mashirika ya ndege ambayo nchi zao zimeshaondolewa vikwazo vya kukaa ndani kutokana na corona kuja kutembea Zanzibar," alisema. Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mauzo wa Kundi la kampuni za Lufthansa Kusini na Mashariki mwa Afrika, Dk. Andre Schulz, alisema kundi la kampuni za Lufthansa limepanua wigo wake Tanzania, ambapo litatoa huduma za ndege mara sita kwa wiki kuunganisha Kilimanjaro, Dar es Salaam na Zanzibar kwa kutumia ndege zake mbili.

Aidha alieleza kuwa ndege mpya ya kisasa ya kundi la kampuni za Lufthansa, Eurowings Discover ilitua na kugusa ardhi ya Tanzania kwa mara ya kwanza ambapo iliruka kuanza safari yake ya kwanza ya abiria kutokea Frankfurt Julai 24, mwaka huu.

Aidha alisema kuwa Zanzibar imekuwa kivutio maarufu kwa wasafiri wengi toka sehemu mbalimbali duniani na wateja wao watakuwa na fursa zaidi za kutembelea visiwa vizuri vya Zanzibar kwa kutumia huduma zao ambazo ni nzuri.

Balozi wa Ujerumani nchini, Regine Hess, alisema, amepata heshima kubwa ya kukaribisha ndege hiyo, ambayo ni ya kwanza kutoka shirika jipya la ndege la Ujerumani la Eurowings Discover.

Aidha alisema ujio wa ndege hiyo ni uamuzi mzuri ambapo shirika linaamini katika kuamsha utalii Zanzibar.




Ndege ya Airbus A330-200 kutoka kampuni ya Eurowings Discover ya Ujerumani ikiwasili kwa mara ya kwanza katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume (AAKIA) Zanzibar, jana ikimwagiwa maji kama ishara ya mapokezi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kongamano kupinga udhalilishaji kijinsia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JUMUIYA ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), inatarajia kufanya kongamano la kitaifa kuhusu udhalilishaji wa kijinsia pamoja na uzinduzi wa mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za kesi za udhalilishaji.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Safia Hija Abras, alisema jumuiya imeandaa mfumo mpya wa ukusanyaji takwimu ili kuipima utendaji kazi katika utetezi wa mauala ya udhalilishaji, ambao utasaidia kuondoa mgongano wakati wa kutoa taarifa za kesi zilizoripotiwa baina ya taasisi moja na nyingine.

Safia alieleza kuwa kila taasisi inayosimamia kupiga vita vitendo vya udhalilishaji itaweza kutumia mfumo huo ili kuepuka kujirejea kwa taarifa wakati wa uwasilishaji wa kesi hizo. "Katika utendaji wa kazi zetu tumeona ili tuweze kupima na kujipima jinsi gani utetezi unafanyika katika masuala ya udhalilishaji ni vyema kuwa na mfumo maalum ambao utakuwa unakusanya data hii itaepusha utofauti wa kuripoti kiwango cha taarifa za udhalilishaji kutoka taasisi moja na nyengine," alisema. Mwenyekiti huyo alisema kupitia kungamano hilo, watapata nafasi ya kutoa taarifa za utekelezaji, mafanikio na changamoto wanazokumbana nazo kuanzia kipindi cha Januari hadi sasa katika kuhakikisha kwamba wanafikio lengo la jumuiya la kutokomeza vitendo hivyo.

Naye Mkurugenzi wa ZAFELA, Jamila Mahmoud, alisema jamii imekuwa na mwamko mkubwa wa kufika katika vituo vya sheria kutoa malalamiko ambapo kutoka mwaka 2020 hadi 2021 jumuiya hiyo imepokea kesi zaidi ya 100 za vitendo vya udhalilishaji.

Kongamano hilo ambalo linalotarajiwa kufanyika Julai 28, litajumuisha Asasi za kiraia na taasisi za serikalil ikiwamo Jeshi la Polisi, na watendaji wa Mahakama ambapo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

## Waonywa kuhusu athari za mazingira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI wametakiwa kuchukuwa tahadhari ya kukabiliana na athari za mazingira.

Hali hiyo inatokana na kuwapo kwa kasi ya mabadiliko ya tabianchi ambayo imesababisha maji ya bahari kuingia katika maeneo ya makazi Pemba.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Mazingira Zanzibar, Farhati Ali Mbarouk, wakati wa ugawaji wa miche ya mikoko kwa wakazi wa mikoa miwili ya Pemba ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na mazingira.

Alikitaja kisiwa cha Pemba kuwa miongoni mwa maeneo yaliyoathirika na mabadiliko ya tabia nchi ambapo baadhi ya maeneo yaliyokuwa yakitumika kwa shughuli za kilimo wananchi wake kulazimika kuhama baada ya kuingia maji ya bahari.

Alikitaja Kisiwa cha Panza kilichopo mkoani Pemba pamoja na Mtambwe kuwa vipo katika hatari ya kutoweka kutokana na kasi ya maji ya bahari katika upande wa kaskazini, huku baadhi ya wananchi wakihama na kuhamia maeneo mengine.

''Njia pekee ya kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabianchi ni kuotesha mikoko ambayo ni maalumu kwa ajili ya kuzuia kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya makazi,'' alisema.

Naye Ofisa wa Idara ya Mazingira, Makame Haji Khamis, alisema zaidi ya vijiji 100 katika kisiwa cha Pemba vinavyopakana na bahari wananchi wake wameanza kuotesha mikoko ikiwa ni juhudi za kuzuia kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya makazi.

''Wananchi wa vijiji vinavyoishi watu pembezoni mwa bahari wameitikia wito wa kuotesha mikoko kwa wingi kwa ajili ya kuzuia kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya makazi,'' alisema Khamis.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mazingira Zanzibar, Sheha Mjaja Juma, aliwataka wawekezaji wanaojenga miradi ya hoteli za kitalii kuzingatia masharti ya uwekezaji ikiwamo kuacha kujenga nyumba za hoteli karibu na fukwe.

Alieleza kuwa wapo wawekezaji wamekiuka masharti ya uwekezaji na kusababisha malalamiko kwa wananchi kwa kuweka matuta na mawe makubwa kuzuia kasi ya maji, lakini matokeo yake maji yote yanakwenda katika maeneo ya makazi ya wananchi na kusababisha athari.

# Mwigulu awatuliza wakazi Tunduma

**Na Benny Mwaipaja, TUNDUMA**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amewahakikishia wakazi wa Mji wa Tunduma, wilayani Momba mkoani Songwe kwamba serikali itatoa Sh. bil. 17 kwa ajili ya mradi wa kusambaza maji katika mji huo kutoka chanzo cha maji cha Mto Bupigu, kilichoko Wilaya ya Ileje.

Dk. Nchemba alisema hayo Mjini Tunduma wakati akizungumza na mamia ya wakazi wa mji huo wakiwamo wafanyabiashara katika mpaka huo wa Tanzania na Zambia.

"Mama yetu Rais Samia Suluhu Hassan amedhamiria kumtua ndoo mama kichwani kwa kuipa kipaumbele sekta ya maji, nimepokea maelezo yenu sisi watendaji wake ni kutekeleza ahadi alizowaahidi," alisema.

Alifafanua kuwa wizara itahakikisha inatoa kiasi hicho cha fedha ili wananchi hao wapate maji na kwamba lengo la serikali ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2025 upatikanaji wa maji mijini unafikia wastani wa asilimia 95 na vijijini asilimia 85.

Dk. Nchemba aliwajibu wananchi hao waliolalamikia kupanda kwa bei ya mbolea kwamba serikali inalifanyiakazi suala hilo na kwamba wataalamu wa Sekta ya Kilimo na Wizara ya Fedha na Mipango wanapitia na kuyafanyiakazi masuala mbalimbali ya kisera yatakayosaidia kupungua kwa bei hiyo.

"Kupanda kwa bei ya mbolea hakutokani na kodi na tozo zilizoongezwa kwenye bajeti hii bali inatokana na kupanda kwa bei huko inakozalishwa nje ya nchi," alisisitiza.

Aliwataka wafanyabiashara wanaohamia Zambia kurejea na kufanyabiashara nchini, na kuwahakikishia kuwa malalamiko yao kuhusu kodi yatafanyiwa kazi.

Wito huo ulitokana na baadhi ya wafanyabiashara kueleza kuwa baadhi ya wafanyabiashara wenzao wamehamishia biashara zao upande wa Nakonde nchini Zambia wakidai kuwa kufanya biashara upande huo kuna nafuu ya kodi ikilinganishwa na upande wa Tanzania.

"Wewe ni Mtanzania usiikimbie nchi yako, tutarekebisha matatizo, lakini kama umepata fursa ya kuwekeza huko, wekeza! Lakini usiikimbie nchi yako kwa sababu ya matatizo. Tanzania inaheshima ya kuzikomboa nchi zote hizi hatuwezi kushindwa kutenda haki kwa wananchi wetu," aliongeza Dk. Nchemba.

# Mabweni mengine yateketea Muleba

**Na Waandishi Wetu**

MOTO mwingine umeteketeza mabweni mawili ya Shule ya Sekondari Jakaya iliyopo Muleba mkoani Kagera.

Tukio hilo limetolea wakati timu ya kuchunguza chanzo cha moto katika Shule ya Sekondari Kiwangwa, wilayani Bagamoyo Mkoa wa Pwani ikitakiwa kufanya kazi kwa weledi ili hatua zichukuliwe kudhibiti matukio ya moto yasijirudie.

Katika Shule ya Jakaya, Mwalimu Suleman akizungumzia tukio hilo alisema wanafunzi wakiwa darasani wakiendelea na kipindi cha dini majira ya jioni Julai 23, mwaka huu, waliona moto kwenye mabweni mawili ya wasichana yenye uwezo wa kupokea wanafunzi 62 kila moja.

"Tuliona moto bweni la kwanza la wasichana ambalo lilikuwa likiungua kwa kasi na kuelekea bweni la pili wakati huo wanafunzi hawakuwa bweninii walikuwa kwenye kipindi cha dini, baada ya kuona hivyo tukifanya ushirikiano wa kuokoa vitu kwenye maneno mengine," alisema Suleman.

Naye Mwalimu wa Taaluma shuleni humo, Ayoub Suleman, alisema walifanikiwa kuokoa mali za wanafunzi ambazo ni magodoro, shuka, vitanda na madaftari.

"Tukitumia vifaa vyetu vya kujikinga na moto tukibeba mchanga, maji wote kwa pamoja uongozi na baadhi ya wanafunzi jasiri tukafanikiwa katika ushirikiano huo mabweni mengine hayakuungua," alisema Suleman.

Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Revocatus Malimi, alithibitisha kutokea kwa tuko hilo na kusema kuwa chanzo hakijafahamika na hakuna madhara kwa binadamu.

Alisema athari kubwa ni kuungua kwa mali za wanafunzi madaftari, magodoro sare za shule vitanda na majengo

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Meja Jenerali Charles Mbuge, alisema aliunda kamati ya kufuatilia kwa kina matukio ya moto.

Wakati huo huo, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, ameagiza timu ya kuchunguza chanzo cha moto katika Shule ya Sekondari Kiwangwa kufanya kazi kwa weledi ili hatua zichukuliwe kudhibiti matukio ya moto yasijirudie.

Kunenge aliyasema hayo jana alipotembelea katika shule hiyo kukagua majengo yaliyoungua na kupokea misaada mbalimbali iliyotolewa kwa wanafunzi wa kike ambao bweni lao liliteketea kwa moto Julai 22 usiku.

"Tumeunda timu kujua chanzo cha moto tujue kama ni upande wa ujenzi wa majengo au hujuma na hii ni kwasababu matukio ya moto yamejirudia katika shule hii," alisema. Kunenge aliwaomba wadau kuendelea kujitokeza kusaidia misaada kwa kadri wanavyoweza ili kukidhi mahitaji kwa vifaa yaliyopo kwa sasa kwa wanafunzi na ujenzi ambao unatarajiwa kuanza.

"Nawashukuru wadau ambao wanaendelea kutusaidia tangu tumepata janga hili la moto, Taasisi ya Miraaj Tanzania na wawekezaji wengine waliopo hapa mkoani kwetu wametusaidia sana lakini bado tunahitaji msaada zaidi," alisema. Aliagiza uongozi wa shule kuwaacha wanafunzi waendelee kuingia darasani hata kama bado hawajapata sare za shule ili waendelee na masomo.

Mbunge wa Jimbo la Chalinze, Ridhiwani Kikwete, alisema uanzishwaji wa mabweni katika Shule za Sekondari kwenye jimbo hilo ililenga kukuza ufaulu.

Naye, Katibu Tawala Wilaya ya Bagamoyo, Kasilda Mgeni, alisema Halmashauri ya Chalinze imewanunulia daftari na kalamu wanafunzi ili waendelee na masomo, huku RC akifanikisha kupatikana kwa mablaketi, vyandarua, magodoro kupitia wafadhili.

Mgeni alisema kwa sasa zinahitajika sare za shule, tisheti, na trakauti, vitanda 48, vitabu 170, masanduku ya kuhifadhia vifaa 170, viatu vya shule pea 170 na soksi.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Miraaj Tanzania, Arif Surya, alisema pamoja na misaada ya magodoro, shuka na mito ambayo wametoa, wataendelea kusaidia mahitaji ambayo hayajakamilika.

Mkuu wa Shule ya Kiwanga, Robad Kibonde alisema bweni hilo la wasichana liliwaka moto Julai 22, mwaka huu, majira ya saa moja usiku wanafunzi wakiwa kwenye vipindi vya dini.

Kibonde alisema kwasasa wanafunzi hao 96 ambao ni wa kidato cha kwanza na cha pili wanalala katika vyumba vya madarasa vitatu hadi pale bweni lao litakapokamilika kujengwa.

***Restuta Damian (MULEBA) na Julieth Mkireri (BAGAMOYO)***



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, akimsikiliza Mhifadhi wa Mambo ya Kale, Mwita William (kushoto), alipokuwa akitoa maelezo kuhusu idara yake wakati wa Tamasha la Majimaji Serebuka linaloendelea katika Uwanja wa Majimaji, Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma. Kulia ni Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Pololeti Mgema. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania yapewa uenyekiti nchi za ushoroba wa kati

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Mawaziri wa Usafirishaji wa Nchi Wanachama wa Ushoroba wa Kati, limeikabidhi Tanzania kuwa mwenyekiti kwa muda wa mwaka mmoja kuanzia mwaka 2021 hadi 2022.

Uwenyekiti huo umekabidhiwa jijini Dar es Salaam kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho kutoka kwa Waziri wa Miundombinu wa Rwanda, Balozi Claver Gatete katika kikao chao cha 11 kilichofanyika kwa njia ya mtandao.

Taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini ilieleza kuwa Dk. Chamuriho alikabidhiwa uenyekiti huo katika kikao hicho kinachojumuisha mawaziri wa usafirishaji kutoka nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Rwanda, Tanzania.

Nchi hizo ni wanachama wa Taasisi ya Ushoroba wa Kati yenye makao yake makuu jijini Dar es Salaam.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa katika kikao hicho mawaziri wamekubaliana kuendeleza na kuimarisha miundombinu ya nchi wanachama kwa kujenga na kuimarisha usafiri katika sekta ya maji, reli, barabara na kuhakikisha Bandari ya Dar es Salaam inaboreshwa ili kuondoa ucheleweshaji wa shehena ya mizigo kwenda nchi wanachama.

Ilieleza kuwa umoja huo pia ulizindua mpango mkakati wa taasisi wa ushoroba wa kati wa miaka mitano (2021 -2025) ambao utaangazia njia zote za usafirishaji.

Ilieleza kuwa miradi iliyoingizwa katika mpango huu ni ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kipande cha Uvinza-Musongati (km 240), ujenzi na ukarabati wa Bandari za Bujumbura, Rumonge na Kabonga nchini Burundi na ujenzi wa barabara ya kimataifa kati ya Tanzania na Burundi kuanzia Rumonge- Gitaza- Kabingo- Kasulu hadi Manyovu.

Ilitaja miradi mingine ni pamoja na reli ya kisasa kutoka Isaka hadi Kigali, ujenzi wa mizani za kupimia mizigo nchini Rwanda, ujenzi na ukarabati wa bandari mbalimbali nchini DRC, ujenzi wa meli ya mizigo kwenye Ziwa Victoria.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa uenyekiti, Dk. Chamuriho alisema serikali imeshasaini mikataba mitano ya ujenzi na ukarabati wa meli.

Kuhusu usafirishaji wa njia ya reli, Dk. Chamuriho, alisema ujenzi wa reli ya kisasa sehemu ya Mwanza hadi Isaka umeshaanza na unatarajiwa kukamilika mwaka 2024.

# Wanafunzi maelfu wakwama Tigray

**Tigray, ETHIOPIA**

HALI katika Jimbo la Tigray imeendelea kuzua wasiwasi mkubwa, wakati watu na wanafunzi kadhaa wamekwama katika jimbo hilo linalokabiliwa na mapigano kati ya waasi wa TPLF na vikosi vya Ethiopia.

Wazazi wanasema hawana taarifa kuhusu watoto wao wanaosomea katika mkoa huo kwa karibu mwezi mmoja.

Wanafunzi katika vyuo vikuu vinne vya umma hawawezi tena kuwasiliana na familia zao.

Wazazi wa wanafunzi hao wanaomba msaada wa kuwaondoa watoto wao katika Jimbo laTigray.

Tangu vikosi vya waasi kutoka Tigray kudhibiti mji wa Mekele, mitandao ya mawasiliano imekatwa tena na barabara nyingi katika mkoa huo zimefungwa.

Wakati huo huo kumeripotiwa uhaba wa chakula.

Kwa jumla, zaidi ya watu milioni tano wanahitaji msaada wa haraka wa kibinadamu, kulingana na Umoja wa Mataifa ((UN).

Mamia kadhaa ya wazazi walikusanyika Ijumaa mbele ya ofisi ya Umoja wa Mataifa huko Addis Ababa, wakiomba Umoja wa Mataifa kuingilia haraka ili kuwaokoa watoto wao waliokwama katika Jimbo la Tigray.

Chuo kikuu chatoa wito kwa serikali kuchukua hatua, mapema mwezi huu, Wizara ya Sayansi na Elimu ya Juu iliwatuliza nyoyo wazazi hao, ikisema kupitia Facebook kwamba wanaendelea na masomo kama kawaida.

Lakini Alhamisi, Chuo Kikuu cha Mekele kilitoa taarifa ya kutatanisha. Wakati chuo hicho kikuu kinafadhiliwa na serikali ya Ethiopia, kilibaini kwamba hakijapokea fedha yoyote kwa mwaka huu.

Chuo pia kinakosa pesa za kuwalisha wanafunzi na akaunti za benki zimezuiwa, hakuna ununuzi wa chakula unaowezekana.

Chuo hicho kilisema kuwa hakitaweza kuchukua jukumu la kuwalisha wanafunzi kuanzia Julai 27.

Chuo kikuu kinatoa wito kwa mamlaka ya Ethiopia kupata suluhu ya hali hiyo kabla ya tarehe hiyo, ama kutuma pesa zinazohitajika au kutuma mabasi ili kuwahamisha wanafunzi kutoka Jimbo la Tigray.

*RFI*




Mjini Paris nchini Ufaransa, waandamanaji walijitokeza barabarani na kusababisha vurugu kwenye mitaa kadhaa kupinga chanjo Covid-19 kuwa lazima. **PICHA: DW**

# Ulaya wapinga sera ya chanjo lazima Covid-19

**Paris, UFARANSA**

MAELFU ya raia kwenye mataifa kadhaa ya Ulaya wameandamana mwishoni mwa wiki kupinga vizuizi vya kudhibiti kusambaa ugonjwa wa Covid-19 na sera za kuwalazimisha kudungwa chanjo.

Raia hao kwenye mataifa ya Ufaransa, Italia na Ugiriki walimiminika mitaani hususani katika miji mikuu ya nchi hizo kupaza sauti ya kupinga kulazimishwa kuchoma chanjo za Covid-19 pamoja na cheti cha kidijitali kwa wale waliopatiwa chanjo.

Wengi walioandamana wanadai sera hizo zinatishia uhuru wa raia katika wakati serikali barani Ulaya zinazidisha shinikizo dhidi ya watu ambao hawajapatiwa chanjo.

Nchini Ufaransa, kiasi watu 160,000 walijitokeza kuonyesha gadhabu zao dhidi ya Rais Emmanuel Macron na serikali yake mjini Paris na katika miji mingine.

Waandamanaji hao wamekasirishwa na muswada mpya wa sheria unaowalazimisha raia kuwa na hati maalumu ya kuthibitisha, wamechanjwa au kuonyesha hawana maambukizi ya virusi vya corona ili kuingia kwenye migahawa na maeneo mengine ya umma.

Nchini Italia kupinga sera za afya za serikali wakati kukianzishwa sheria kali za kudhibiti kuenea kwa virusi vya corona.

Shirika la Habari la ANSA limeripoti kuwa watu elfu tatu walikusanyika kwa maandamano dhidi ya cheti cha kidigitali cha corona cha Umoja wa Ulaya(EU), kinachojulikana Italia, kama pasi ya kijani.

Gazeti la Corriere della Sera, limeripoti kuwa maandamano yalifanyika katika miji ya Milan, Turin na Naples.

Serikali ya Italia imeimarisha hatua za kupambana na ongezeko la visa vya maambukizi ya virusi vya corona huku ikiweka masharti makali kwa mikusanyiko kwenye maeneo ya ndani.

Kuanzia Agosti 6, mwaka huu, watu watahitajika kutoa uthibitisho wa chanjo, matokeo yanayothibitisha kutoambukizwa virusi hivyo ama ushahidi wa kupona baada ya maambukizo.

Ili kushiriki katika dhifa za chakula za ndani ama kuingia katika makavazi na mabwawa ya kuogelea miongoni mwa maeneo mengine ya umma.

*DW*

## Uingereza mwenyeji mkutano dunia mabadiliko ya tabianchi

**London, UINGEREZA**

UINGEREZA imeandaa mkutano wa mawaziri wa mazingira na hali ya hewa kutoka mataifa 51 kwa mazungumzo muhimu ya hali ya hewa kabla ya mkutano wa kilele wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi COP26 utakaoandaliwa Novemba mjini Glasgow nchini Scotland.

Waziri wa Mazingira wa Uingereza, Alok Sharma ambaye ndiye rais wa COP26 ataongoza mkutano huo wa siku mbili ambao Uingereza inasema kuwa utashughulikia masuala muhimu yanayohitaji kupata maazimio wakati wa mkutano huo wa mjini Glasgow.

Mawaziri wa mazingira na hali ya hewa kutoka Marekani, India na China watakuwa miongoni mwa wale watakaoshiriki katika mkutano huo wa faragha utakaofanyika kwa njia ya video na pia ana kwa ana.

Huu ni mkutano wa kwanza wa aina hii wa mawaziri utakaoandaliwa ana kwa ana baada ya muda wa zaidi ya miezi 18 kutokana na janga la virusi vya corona.

**DW**

## Wanajeshi sita wauawa kwa shambulizi la Boko Haram

**Sagme, CAMEROON**

WANAJESHI sita wa Cameroon wameuawa Jumamosi mwishoni mwa wiki katika shambulio la Boko Haram Kaskazini mwa nchi, wanajihadi wameongeza mashambulizi, gavana wa mkoa huo amesema kwenye televisheni ya serikali.

Boko Haram walifanya shambulio kwenye kituo cha jeshi huko Sagme, karibu na mpaka na Nigeria, Kaskazini mwa nchi hiyo, Jumamosi asubuhi.

Eneo ambalo Boko Haram imekuwa ikitekeleza mara kwa mara mashambulizi.

Gavana wa Mkoa wa Kaskazini amewataka raia kushirikiana na vikosi vya ulinzi na usalama kwa kuwafichua wapiganaji na wanamgambo wa kundi la Boko Haram na wahalifu wengine.

**RFI**

# JUVENTUS yaridhia kumwachia Ronaldo




**TURIN, Italia**

KLABU ya Juventus ipo tayari kumwachia mshambuliaji wao nyota, Cristiano Ronaldo kujiunga na PSG, ili wao waipate saini ya Mauro Icardi.

Kocha wa Juventus, Massimiliano Allegri ameweka wazi anahitaji huduma ya Icardi kwenye kikosi chake kwa ajili ya msimu ujao.

Na mabosi wa Juventus wanapambana kuinasa saini yake, huku PSG wao wakiweka wazi wanamhitaji Ronaldo.

Mfungaji huyo bora wa michuano ya Euro 2020 hivi karibuni aliweka wazi hataki kusalia ndani ya kikosi cha Juventus, licha ya kwamba mpaka sasa amebakiwa na mkataba wa mwaka mmoja ndani ya kikosi cha timu hiyo na kama ataenda PSG basi ataungana na Mbrazili, Neymar Junior.

Nyota huo ambaye ana miaka 36 kwa sasa anaonekana kukosa furaha ndani ya Juventus hasa baada ya kukosa taji la ubingwa wa Ligi Kuu Italia msimu huu.

## BAYERN YAMTAKA SERGI WA BARCA




**MUNICH, Ujerumani**

BAYERN Munich imeripotiwa kuwa na nia na iko katika mazungumzo kumsajili Sergi Roberto kutoka Barcelona kwa mkopo msimu huu wa kiangazi.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, wanajaribu kuimarisha safu yao ya ulinzi na kocha mpya Julian Nagelsmann anasemekana amemtambua raia huyo wa Hispania kama chaguo muhimu kwake.

Ripoti zimesema Barcelona itakuwa tayari kuidhinisha uhamisho iwapo tu utahusisha chaguo la kumnunua mchezaji huyo mwisho wa mkopo.

Mkataba wa sasa wa Roberto pale Nou Camp unamalizika msimu ujao wa majira ya joto na Barca ambayo ina uhaba wa fedha haitamruhusu kuondoka bila ada.

Barcelona inahitaji kufuta pauni milioni 156 sawa kutoka kwenye bili ya sasa ya mshahara wa wachezaji.

Kikomo chao kilikuwa pauni milioni 296 mwaka uliopita na sasa kimeshushwa hadi pauni milioni 136.

## Odoi akataa kuondoka Chelsea

**LONDON, England**

WINGA wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi ameripotiwa kukataa mpango wa kufanywa chambo ya kubadilishwa na nyota wa Bayern Munich, Kingley Coman

Mabosi wa Chelsea wanataka kumtumia Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 20, kama sehemu ya mabadilishano ya kuipata saini ya Coman mwenye miaka 25.

Dili hilo lilipangwa kufanywa wakati huu wa dirisha la majira ya joto, lakini Hudson-Odoi mwenyewe anataka kuendelea kusalia kwenye kikosi na kupigania nafasi yake.

Mkataba wa Odoi unamalizika mwaka 2024 na haonekani kuwa kwenye mipango ya kocha, Thomas Tuchel kwa msimu unaokuja.

Msimu uliopita alicheza mechi 37 za michuano yote na kufunga mabao matano, lakini kati ya hizo kwenye Ligi Kuu England alicheza mechi 23 pekee.

Tuchel amekuwa bize kujenga kikosi chake kwa msimu ujao ambapo anahitaji pia kuipata saini ya nyota wa Borrussia Dortmund Erling Haaland.



HABARI MICHEZO



# SOLSKJAER ASAINI MKATABA MPYA

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesaini mkataba mpya na klabu hiyo utakaomweka hadi mwaka 2024, huku kukiwa na kipengele cha kuongeza mwaka mmoja zaidi.

Raia huyo wa Norway mwenye umri wa miaka 48, alipewa mkataba wa kudumu Machi mwaka 2019, baada ya kuwa kocha wa muda wakati Jose Mourinho alipofukuzwa miezi mitatu mapema.

Aliiongoza United kumaliza nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu msimu uliopita na kucheza fainali ya Ligi ya Europa, ambapo walipoteza.

Solskjaer alisema "nimefurahishwa" kusaini mkataba mpya.

"Tunajiamini zaidi kuliko mwanzo, chini ya uongozi wa Ole, tunakwenda njia tofauti na sahihi," alisema Makamu Mwenyekiti Mtendaji wa Manchester United, Ed Woodward.

"Ole na benchi lake la ufundi wamefanya kazi bila kuchoka na kwa hakika tunaimani atakuwa na muda mrefu wa mafanikio hapa."

Solskjaer alitumia misimu 11 akiwa mchezaji hapo United, akifunga bao la ushindi kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 1999 dhidi ya Bayern Munich.

Amekuwa kocha wa nne kusaini mkataba wa kudumu baada ya Sir Alex Ferguson ambaye alistaafu mwaka 2013 wakati aliposaini mkataba wa miaka minne Machi mwaka 2019.

## KLOPP HANA HARAKA NA VAN DIJK, GOMEZ

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amebainisha kwamba, Virgil van Dijk na Joe Gomez wanaonekana "wako vizuri" kwenye mazoezi ya maandalizi ya msimu mpya na Liverpool, ingawa aliweka wazi kwamba atatakiwa kuwa mvumilivu juu ya kurudi dimbani kwa wawili hao.

Van Dijk na mlinzi mwenzake wa kati, Gomez kwa muda mrefu walikuwa nje ya dimba wakati wekundu hao wakiwa na safu ya ulinzi dhaifu kwenye msimu ulioisha wa 2020-21, wakiwa wamecheza mechi 12 kwa ujumla za Ligi Kuu.


Wote wawili wanakaribia kurudi dimbani, lakini Klopp alisisitiza baada ya ushindi wa 1-0 kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Mainz Ijumaa kwamba, hatakuwa na haraka ya kuwarejesha uwanjani.

Alipoulizwa na waandishi wa habari kama walinzi hao watacheza kwenye mchezo wa Alhamisi ijayo, alijibu: "Pengine, inaweza kuwa mshangao, lakini kwa hakika wanaonekana wako vizuri.

"Wanaonekana wanaweza kucheza, lakini hapa ni kwenye mazoezi, hatuwezi kufanya haraka warejeaa dimbani, tutaangalia kwanza nini kilichopo kwao na kama wako fiti."

"Tunatakiwa kuwa wavumilivu - tunajiandaa kwa ajili ya msimu mzima, sio kwa mechi za maandalizi tu ya msimu. Haitakuwa hatari kwa mchezo mmoja hapa, lakini tutaangalia.

"Bado tuna mechi nyingi zinakuja, lakini sioni kama wanaweza kuhusishwa kwenye mechi zijazo."



## BARCELONA YAJIPANGA KUMUUZA GRIEZMANN

**BARCELONA, Hispania**



BARCELONA inafikiria makubaliano ya kubadilishana mshambuliaji, Antoine Griezmann na Paulo Dybala wa Juventus wakati huu wakipambana kupunguza bili ya mshahara wa klabu hiyo.

Gazeti la kila siku la Ufaransa, L'Equipe limesema klabu hiyo ina nia kumuuza Griezmann ambaye anapata mshahara wa pauni 300,000 kwa wiki pale Nou Camp.

Timu hiyo ya LaLiga iko katika matatizo ya kifedha na inajitahidi kuondoa wachezaji kadhaa ili kusajili wengine na kumsainisha tena Lionel Messi mkataba mpya.

Dybala mwenye umri wa miaka 27 ambaye amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake Juventus alikuwa na msimu mchanganyiko katika Serie A kipindi kilichopita wakati klabu hiyo ilipopoteza ubingwa wa Italia akifunga magoli matano na kutoa pasi tatu za mwisho.

Tangu ujio wa Cristiano Ronaldo pale Juventus, Dybala anaonekana kutokuwa kwenye kiwango cha kuvutia kama misimu ya nyuma.

Na sasa Barcelona wanaona kwamba, Dybala anaweza kufiti kwenye mfumo wake akicheza sambamba na raia mwenzake wa Argentina, Messi.

HABARI MICHEZO

## KWA UFUPI

### JUVE YAIKATALIA LIVERPOOL

KLABU ya Juventus imekataa dau la pauni milioni 86 kutoka kwa Liverpool kwa ajili ya kumsajili, Federico Chiesa. Winga huyo mwenye umri wa miaka 23, alikuwa mchezaji nyota wa Italia katika michuano ya Euro 2020. ***(Repubblica)***

### CORREA AWANIWA EPL

ARSENAL, Tottenham na Everton zinawania kumsajili nyota wa Argentina, Joaquin Correa mwenye umri wa miaka 26, ambaye anatarajiwa kuondoka Lazio msimu huu. ***(Corriere dello Sport)***

### MARTIAL KUUZWA

MANCHESTER United inaweza kumuuza mshambuliaji wa Ufaransa, Anthony Martial mwenye umri wa miaka 25, huku Tottenham wakionyesha nia ya kumtaka. ***(Star)***

### POGBA ATAKIWA KUBAKI

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, anataka kiungo wake wa kati, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28, kubakia katika klabu hiyo, huku Paris St-Germain ikimtaka . ***(Manchester Evening News)***

### WIJNALDUM HAKUPENDWA

KIUNGO wa kati wa PSG na Uholanzi, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30, amesema "hakuhisi kupendwa" na mitandao ya kijamii na ilianza kumkosoa kabla ya kuondoka kwake Liverpool, Juni. ***(Observer)***

### WHITE RASMI ARSENAL

ARSENAL inatumaini kuthibitisha kumsajili Ben White mwenye umri wa miaka 23 kwa pauni milioni 50, kutoka klabu ya Brighton baada ya kufanyiwa vipimo vya afya wikendii. ***(Mail)***

### ZAKARIA HUYO ARSENAL

ARSENAL inaangalia uwezekano wa kumsajili kiungo wa kati wa Uswizi, Denis Zakaria mwenye umri wa miaka 24, ambaye ameelezea nia yake ya kuondoka Borussia Monchengladbach. ***(Mirror)***

### KANE KACHOKA

NAHODHA wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27, anatarajiwa kukosa mwanzo wa msimu wa Ligi Kuu ya England kutokana na uchovu baada ya michuano ya Euro 2020.***(Telegraph)***

### ARMSTRONG AOTA MBAWA

DAU la Watford la pauni milioni 15 kwa ajili ya Adam Armstrong mwenye umri wa miaka 24, limekataliwa, huku Blackburn wakitaka kumuuza mshambuliaji huyo wa zamani wa kikosi cha England cha chini ya umri wa miaka 21 kwa pauni milioni 25. ***(Sun)***

### GERRARD ASHANGAA

KOCHA wa Rangers na aliyekuwa nahodha wa Liverpool, Steven Gerrard mwenye umri wa miaka 41 amesema alishangazwa baada ya kuhusishwa na kazi ya kuinoa Everton kabla ya kuteuliwa Rafael Benitez na kwamba mpango kama huo hauwezekani. ***(ESPN)***

### VILLA YAKATALIWA KWA BAILEY

KLABU ya Bayer Leverkusen imekataa dau la pauni milioni 30 kutoka kwa Aston Villa ili kumuuza winga wa Jamaica mwenye umri wa miaka 23, Leon Bailey. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SANCHO: NDOTO YANGU IMETIMIA KWA MAN U

●●●Aishukuru Dortmund kumpa nafasi na alijua atarudi England kwa...

**MANCHESTER, ENGLAND**

WINGA wa England, Jadon Sancho amesema kwamba, kujiunga na Manchester United ni ndoto iliyotimia baada ya kukamilisha uhamisho kutoka klabu ya Borussia Dortmund kwa dau la pauni milioni 73, mapema juzi.

Sancho ndiye mchezaji wa pili wa England mwenye thamani ya juu baada ya mchezaji mwenza wa United, Harry Maguire na amesaini mkataba wa miaka mitano kuichezea klabu hiyo.

"Naishukuru Dortmund kwa kunipatia fursa ya kucheza katika kikosi cha kwanza, ingawa nilijua kwamba nitarudi England," alisema Sancho mwenye umri wa miaka 21.

"Fursa ya kujiunga na Manchester United ni ndoto iliyotimia na sasa nasubiri kuonyesha umahiri wangu katika Ligi Kuu ya England, EPL."

"Hiki ni kikosi kichanga na najua, pamoja tunaweza kujenga kitu maalum ili kuleta ufanisi ambao mashabiki wanahitaji."

United waliafikia makubaliano ya kumsajili Sancho Julai Mosi, mwaka huu na kandarasi yake ya miaka mitano na klabu hiyo ina kifungu cha kuongezewa miezi mingine 12.

Ukamilishaji wa makubaliano hayo unasitisha uwindaji wa kumsajili mchezaji huyo. Walitarajiwa kumsajili msimu uliokwisha lakini wakatofautiana kuhusu dau la uhamisho wake.

Sancho alifunga mabao 50 na kutoa usaidizi wa magoli 57 katika mechi 137 alizochezea Dortmund.

Kocha wa Man United, Ole Gunnar Solskjaer amesema kwamba Old Trafford itampatia Sancho fursa anayohitaji kuonyesha kipaji chake.

"Jadon ni aina ya mchezaji ambaye nilipenda kumleta katika klabu hii - ni mshambuliaji anayeingiliana na utamaduni wa Manchester United," alisema Solskjaer akiiambia tovuti ya klabu hiyo.

"Atakuwa kiungo muhimu wa kikosi changu kwa miaka kadhaa ijayo na tunatarajia kwamba atang'ara.

"Mabao yake na rekodi yake ya usaidizi ni ya kipekee na pia atatuongezea kasi katika mchezo wetu, umahiri na ubunifu katika timu."

Kurudi kwa Sancho katika Ligi ya England kunajiri baada ya kuisaidia timu ya taifa kufuzu katika fainali ya kombe la Euro 2020, ambapo walifungwa na Italia kwa changamoto ya mikwaju ya penalti.

Mchezaji huyo wa zamani wa kikosi cha vijana cha timu ya Manchester City pamoja na Bukayo Saka na Marcus Rashford walikabiliwa na ubaguzi wa rangi katika mitandao ya kijamii baada ya kushindwa kufunga penalti muhimu walizopewa.

HABARI MICHEZO

# KIGOMA SISTERS YAITUPIA LAWAMA SIMBA QUEENS

**Na Somoe Ng'itu, KIGOMA**

CHAMA cha Soka cha Mkoa wa Kigoma (KFA), kimesema kuanguka kwa timu yao ya wanawake ya Kigoma Sisters kulitokana na kuibuka kwa timu za Simba Queens na Yanga Princess zote za jijini Dar es Salaam.

Kigoma Sisters ilikuwa ndio mshindani wa karibu wa Mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Mlandizi Queens ya Pwani katika msimu wa 2015/16.

Baada ya msimu huo, Kigoma Sisters iliondokewa na wachezaji wake mahiri na msimu uliopita ilikuwa na hali mbaya ya kupambana isishuke daraja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa KFA, Omary Gindi alisema wameanza mikakati ya kusajili wachezaji wengine wenye uwezo ili kuirejeshea makali timu yao kwa ajili ya msimu mpya wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Gindi alisema wameandaa kamati maalum ambayo itasimamia mchakato wa usajili na programu mbalimbali za mazoezi ili kukijenga imara kikosi chao.

"Ujio wa Simba na Yanga wanawake ulituumiza sana, walikuja na nguvu kubwa ya kusajili wachezaji, wakatuacha taabani, ilikuwa ni changamoto kubwa sana kwetu na klabu nyingine ambazo hazina nguvu ya kupambana nao," alisema Gindi.

Aliongeza wanaamini mikakati waliyoipanga itasaidia kuirejesha timu yao kwenye ushindani na hatimaye kupa mkoa wao heshima ya kuwakilishwa vyema kwenye Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Simba Queens ndio Mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ambao wameshinda taji hilo kwa mara ya pili mfululizo.



Viongozi na wanachama wa Simba wakiwa na watoto wa kituo cha Sanganigwa baada ya kuwapatia msaada wa vitu mbalimbali walipokwenda kutembelea kituo hicho, juzi. Pia walitoa msaada katika kituo kingine cha Maendeleo Brothers. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# Mtibwa sasa yajikita kwenye usajili

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kubaki katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Mohammed Badru, amesema yuko makini katika usajili wa wachezaji na kufanya maandalizi mazuri kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mtibwa Sugar imefanikiwa kubaki katika ligi, baada ya kupata matokeo mazuri katika michezo yake miwili ya Play Off kwa kumfunga Transit Cape FC.

Akizungumza na gazeti hili jana, Badru alisema atakabidhi ripoti yake itakayoeleza nafasi anazotaka kusajili kwa lengo la kuboresha kikosi chake kuelekea msimu.

Alisema alipofika Mtibwa Sugar ni mwishoni mwa msimu na kufanikiwa kuibakiza katika ligi sasa anahitaji kuimarisha kwa kufanya usajili kulingana na mahitaji ya timu yake na kufanya vizuri kwa msimu ujao.

**"Msimu huu ulioisha haukuwa mzuri kwa Mtibwa Sugar, tumeona upungufu, nina imani tu nafanyia kazi pungufu wetu ikiwamo usajili wa wachezaji wapya na ku wapandisha wachezaji kutoka kikosi cha vijana," alisema.**

Alisema anafurahi wachezaji wamepambana katika michezo miwili ya Play off na kuendelea kubaki katika ligi hiyo kwa msimu ujao na kuhakikisha makosa yaliyojitokeza msimu huu, kutojirudia kwa msimu ujao.

# Azam yataja sababu ya kuwaacha wa kimataifa

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC, umetoa sababu ya kuachana na nyota wake wanne wa kimataifa kutokana na kushindwa kupata namba ndani ya kikosi cha kwanza kwa msimu uliopita wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Azam imeachana na beki wa kati, Yakubu Mohammed, kiungo Ally Niyonzima, mshambuliaji, Mpiana Monzinzi walioingia makubaliano ya kuvunjiwa mkataba na Obrey Chirwa ambaye mkataba wake umemalizika.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zakaria, alisema uamuzi wa kuachana na nyota hao ni baada ya mapendekezo ya Kocha Mkuu, George Lwandamina kutokuwa katika mipango yake kwa msimu ujao. Alisema wanawashukuru kwa mchango wa nyota wao walioutoa katika timu hiyo kwa kipindi chote kulingana na mahitaji ya benchi la ufundi na kushindwa kupata nafasi ndani ya timu wameamua kuachana nao.

"Hivi karibuni wamekosa nafasi ya kucheza ndani ya kikosi cha kwanza, kulingana na wao wachezaji wa kigeni tumeona busara kuachana nao ili kwenda kutafuta timu nje ya Azam FC ili kulinda vipaji vyao."

"Kuondoka kwao hao kunatoa nafasi ya waliosajiliwa kulingana na mapendekezo ya kocha Lwandamina kuchukuwa nafasi zao, kwa lengo la kuimarisha kikosi chetu kuelekea msimu ujao," alisema Zakaria.

Alisema wachezaji waliosajiliwa ni mapendekezo ya kocha huyo ambaye wengi wao aliwakilisha majina ya nyota hao na wengine nafasi kulingana na mahitaji yao kwa msimu ujao.

"Msimu ujao tuna nafasi ya kucheza kombe la Shirikisho Barani Afrika (FA), tunapaswa kusajili wachezaji ambao watasaidia timu kwa ajili ya kufikia malengo katika michuano hiyo pamoja na kufanya vizuro katika ligi yetu ya nyumbani," alisema Zakaria.

Uongozi wa Azam FC tayari umewatambulisha nyota watano, wanne wa kimataifa ambao ni Mshambuliaji wa kimataifa wa Zambia, Rodgers Kola (Zanaco), kiungo mshambuliaji wa Zambia na Cape Town City ya Afrika ya Kusini, Charles Zulu.

wengine ni kiungo mshambuliaji wa Kenya, Kenneth Muguna (Gor Mahia), kiungo mkabaji wa Zambia, Paul Katema, (Red Arrows) na beki iwa kushoto wa kimataifa wa Tanzania, Edward Manyama kwa usajili huru akitokea Ruvu Shooting.

# Michezo

Jumatatu Julai 26, 2021
Nipashe



**Sancho: Ndoto yangu imetimia kwa Man U** HABARI UK. 22



Wachezaji wa Simba wakishangilia kombe la Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), baada ya kulitwaa jana kwa kuifunga Yanga bao 1-0 kwenye mchezo uliopigwa Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# SIMBA BINGWA FA

## ●●●Yalipa kisasi kwa watani zao wakati Tonombe akiipa pancha Yanga kwa kulimwa kadi nyekundu...

**Na Waandishi Wetu, KIGOMA**

BAO pekee lililofungwa na Mganda, Thadeo Lwanga jana liliifanya Simba kulipiza kisasi cha kufungwa Julai 3, kwenye mechi ya Ligi Kuu, kwa kuwatwanga watani zao wa jadi Yanga bao 1-0 na kutwaa Kombe la Shirikisho la Soka Tanzania, maarufu kama FA, kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma jana.

Lwanga aliunganisha mpira kwa kichwa kwa kona iliyopigwa na Luis Miquissone na mpira ukawapita mabeki wa Yanga na kipa wao, ukajaa wavuni.

Ushindi wa Simba dhidi ya Yanga umeifanya timu hiyo kutwaa kombe hilo kwa mara ya pili mfululizo, lakini kuwafunga tena mara ya pili watani wao wa jadi kwenye michuano hiyo.

Ikumbukwe Simba iliifunga Yanga mabao 4-1 kwenye mechi ya nusu fainali Julai 12, mwaka jana, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Katika mchezo huo, Yanga walianza kwa kasi, kwani mpira ulipoanza tu ilipigwa pasi ndefu kwa Tuisila Kisinda ambaye alikimbia kwa kasi na kupiga krosi iliyokosa muunganishaji, sekunde ya 30.

Dakika ya pili, golikipa wa Simba, Aishi Manula aligongana na Ditram Nchimbi kutokana na shambulizi kali langoni mwake dakika hizo za mwanzoni.

Hatimaye Simba ilifika golini kwa Yanga dakika ya 30, baada ya Miquissone kuukimbilia mpira ulioonekana kama unataka kutoka na kupiga krosi iliyomkuta Chris Mugalu akapiga 'tik-tak' ambayo iliwagonga mabeki wa Yanga na kurejea uwanjani.

Dakika sita baadaye Miquissone alikuwa kwenye nafasi nzuri ya kufunga, lakini shuti lake lilimbabatiza Bakari Mwamnyeto na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda.

Kiungo mkabaji wa Yanga, Mukoko Tonombe alitolewa nje kwa kadi nyekundu na mwamuzi Ahmed Aragija dakika ya 45, baada ya kumpiga kiwiko nahodha wa Simba, John Bocco.

Kipindi cha kwanza timu zote zilionekana kucheza mchezo wa pasi ndefu, huku wachezaji wa timu zote mbili wakiwa hawajatulia.

Pia Uwanja wa Lake Tanganyika ulionekana kama mdogo kutokana na mara kwa mara pasi za wachezaji wa timu zote mbili kutoka nje.

Kipindi cha pili Simba iliingia kwa spidi kali na ilikuwa dakika 52, Miquissone alipaisha mpira akiwa kwenye nafasi nzuri baada ya kupewa pasi ya Mugalu.

Yanga nusura ipate bao dakika ya 62 kutokana na shambulizi la kushtukiza, baada ya Yacouba Songne kuupata mpira na kuwalamba chenga mabeki wa Simba, kabla ya kuachia shuti kali lililotoka juu, nje kidogo ya lango.

Mugalu naye aliikosesha Simba bao dakika ya 72, akiwa ana kwa ana na kipa Farouk Shikalo alipopiga shuti lililombabatiza na kutoa kona.

Lwanga, baada ya kukosa bao dakika ya 70, alisawazisha makosa yake kwenye dakika ya 79 na kupeleka furaha Msimbazi.

Pamoja na timu zote kufanya mabadiliko kwa nyakati tofauti, lakini Simba ilifanikiwa kulilinda goli lake kwa dakika 11 zilizobaki.

**KURUSHIANA CHUPA**

Baada ya bao kulikuwa na vita vya kurushiana chupa za maji kati ya mashabiki wa Yanga na Simba.

Na baadhi ya mashabiki wa Yanga wakaamua kuondoka katika jukwaa lao na kwenda nje huku wakisusia mechi.

**FISTON AVULIWA SOKSI**

Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Abdoul alivuliwa soksi na mmoja wa viongozi wa benchi la ufundi la timu yake hiyo, kwa sababu alivaa za rangi nyekundu akiwa tofauti na wachezaji wenzake walivalia rangi nyeusi na njano.

Kitendo hiko kilifanyika muda mfupi wakati vikosi vya timu zote mbili vikiwa uwanjani vinafanya mazoezi mepesi kabla ya kuanza kwa mchezo huo.

**TIMU KUWASILI**

Kikosi cha Simba kiliingia uwanjani saa 8:28 kikiambatana na viongozi wote na baada ya dakika 5 kikosi cha Yanga kiliingia kupitia geti la mashabiki na kuingia katika vyumba vya kubadilishia nguo.

Hadi saa 6:46 na 7:47 mchana, mashabiki wa Simba na Yanga walipoteza fahamu kulingana na hali ya jua kali na msalaba mwekundu walifanya kazi kubwa ya kutoa huduma ya kwanza.

Suala la usalama wa raia na mali zao lilikiwa vizuri baada ya Polisi kuwapo wengi uwanjani asubuhi na mapema kwa ajili ya kufanya majukumu yao ndani na nje ya uwanja.

Mashabiki wa timu zote mbili Simba na Yanga walijitokeza kwa wingi kuanzia saa moja asubuhi kwa lengo la kuwahi kuingia mapema uwanjani kulingana na maelekezo yaliyotolewa na mhusika wa usalama.

Mashabiki walikuwa wengi sana na ilipofika saa 6:00 tayari Simba na Yanga walifanikiwa kujaza majukwaa yote ya Sh. 15,000 na 10,000.

Ilikuwa ni kama Dar es Salaam yote imehamia Kigoma, baada ya mji huko kufurika kwa watu wa mpira wa miguu na wafanyabiashara wa mkoa huo kuona imeingia neema.

**LWANGA MCHEZAJI BORA**

Mfungaji wa bao la Simba, Taddeo Lwanga alichaguliwa kuwa mchezaji bora wa mchezo huo.

***Imeandikwa na Somoe Ng'itu, Saada Akida na Adam Fungamwango.***

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >